
SportPesa

TZS. 823,998,440

NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SHAHIDI** aeleza wenzake Sabaya walikiri kuwapo kupokea rushwa mil. 90/-




UKURASA 11

Nipashe

Ijumaa Januari 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580818

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# ANG'ATUKA

**HATIMAYE** Ndugai atangaza kujiuzulu u- Spika wa Bunge, ni baada ya shinikizo kutoka kila kona...*Endelea ukurasa 2 & 7*

## Mbio za kumrithi Maalim ACT - Wazalendo zaanza

UKURASA 17




Mwanachama wa Chama cha ACT-Wazalendo, Juma Duni Haji (kushoto), akipokea fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa taifa wa chama hicho, kutoka kwa Mjumbe wa Kamati ya Uchaguzi Taifa ya chama, Muhene Said Rashid, Vuga mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**



Job Ndugai

## Nyumba 99 zaezuliwa kwa mvua, upepo mkali

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YATAMBA IMELAMBA DUME** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mvua yajeruhi, yaharibu nyumba 99

**Na Waandishi Wetu**

TAKRIBANI nyumba 99, paa za shule na nyumba za walimu zimeezuliwa wilayani Mbinga na Tunduru mkoani Ruvuma kutokana na mvua iliyonyesha ikiambatana na upepo mkali.

Katika nyumba hizo, 55 ni kutoka katika kata ya Mkako wilayani Mbinga ambako mvua kubwa yenye upepo imesababisha nyumba na paa za shule na nyumba za walimu kuezuliwa, hivyo kusababisha mamia ya wananchi kukosa makazi.

Diwani wa Mkako, Isack Ndunguru, alisema jana kuwa mvua kubwa ikiambatana na upepo mkali ilianza kunyesha juzi majira mchana kwa muda wa saa moja na kusababisha uharibifu mkubwa wa majengo ya wananchi na ya serikali.

Ndunguru alisema majengo yaliyoathirika kutokana na adha hiyo ni pamoja na Shule ya Msingi Mkako ambako imeezuliwa paa za nyumba mbili za walimu, jengo moja lenye madarasa mawili na ofisi ya mtendaji kata.

Kwa mujibu wa diwani huyo, tathmini ya hasara ilitokea bado inaendelea kufanyiwa kazi na uongozi wa serikali na kata ya Mkako.

Alisema nyumba 55 za wananchi katika kijiji hicho zimeezuliwa na kusababisha baadhi ya wananchi kukosa mahali pa kuishi na kwamba watu hao wamehifadhiwa kwa muda kwenye nyumba za majirani na walimu ambao baadhi yao pia ni waathirika na wanaishi kwa walimu wenzao.

Kutokana na janga hilo, diwani huyo ameiomba serikali kupitia ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga kuwasaidia waathirika hao ambao kwa sasa wanahitaji msaada kwa kuwa nyumba zao zinahitaji kukarabatiwa pamoja na kuezekwa.

Baadhi ya waathirika hao walisema kwa sasa wananishi kwenye nyumba za majirani na kwamba wanahitaji msaada wa chakula kwa kuwa nyumba zao zilipoezuliwa, vyakula kama mahindi, unga na nafaka zingine ziliharibika kutokana na kunyeshewa na mvua.

Katika hatua nyingine, mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali katika kijiji cha Tuwemacho wilayani Tunduru, imeezua nyumba 44 na kuwaacha baadhi ya kaya zikiwa hazina makazi.

Licha ya kukosa makazi, pia wananchi watatu walijeruhiwa kutokana na kuangukiwa na matofali yaliyokuwa yakiporomoka kutoka katika nyumba zao.

Diwani wa Tuwemacho, Hadija Timamu, alithibitisha kutokea kwa maafa hayo na kwamba kwa sasa wananchi waliopatwa na mkasa huo wamepewa msaada wanaishi kwa majirani wakati wakifanya marekebisho yaa nyumba zao.

Diwani huyo alisema miongoni mwa nyumba hizo ni pamoja na nyumba tatu za walimu, nyumba 40 za wananchi, matundu 11 ya vyoo vya Shule ya Msingi Tuwemacho na jengo la ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kata hiyo.

Alisema hiyo ni awamu ya pili tangu apate nafasi ya uongozi wake na kwamba tukio kama hilo lilitokea mwaka 2019.

Timamu aliwashukuru Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Haillu Mussa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashsuri, Chiza Marando, kwa kuwatembelea wananchi na kuwapa moyo katika kipindi hiki kigumu wanachopitia kutokana na tukio hilo.

Akizungumzia hali za majeruhi waliokumbwa na mkasa huo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Ally Fadhili, alisema kuwa majeruhi wote walipata majeraha vichwani na miguuni na kwamba walipelekwa katika zahanati ya kijiji na kupatiwa matibabu kisha baadaye kuruhusiwa kurejea nyumbani. Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, alisema amemwagiza Marando kupeleka wataalamu ili wakafanye tathmini ya uharibifu uliojitokeza.

Mtatiro pia alimtaka mkurugenzi huyo kuangalia uwezekano wa kufanya ukarabati wa miundombinu ya shule kwa kutumia fedha zilizobaki kwenye ujenzi wa mradi wa kutumia fedha za mkakati wa kitaifa wa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma kwa jamii inayotekelezwa na serikali.

**Imeandikwa na Gideon Mwakanosya, MBINGA, na Steve Chindiye, TUNDURU**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi na Mkewe Mama Marium Mwinyi, wakipata maelezo kutoka kwa Mwekezaji Rahim Balu (kulia), baada ya kufungua hoteli ya Marijani Resort & Spa iliyoko Pwani Mchangani, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya Miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Ndugai ang'atuka u-Spika

**Na Waandishi Wetu**

HATIMAYE ameng'atuka. Ndivyo hali inavyoweza kuelezwa kutokana na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kutangaza kujiuzulu nafasi hiyo jana.

Ndugai amefikia uamuzi huo baada ya mashambulizi kutoka kila kona tangu aliposema kwamba: "Kuna wakati nchi inaweza kuuzwa kwa sababu ya mikopo ambayo serikali imekuwa ikikopa" kutoka katika taasisi mbalimbali zikiwamo nchi wahisani, Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Tangu wakati huo kumekuwa na majibu juu ya hoja hiyo kutoka kwa viongozi wakuu serikalini pamoja na wakuu wa taasisi za fedha kutetea uamuzi wa serikali juu ya kukopa, sababu kubwa ikielezwa kuwa ni kwa ajili ya maendeleo.

Pamoja na wadai wa masuala ya siasa na jamii kwa ujumla kuona ni wazi hiyo ndiyo sababu ya kuachia ngazi, mwenyewe ameweka bayana katika barua ya kuachia ngazi kwamba ni uamuzi binafsi na hiari ambao ameufanya kwa kuzingatia na kujali maslahi mapana ya taifa.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Ofisi ya Bunge na kutiwa saini na Spika huyo, ilieleza pia amezingatia maslahi mapana ya serikali na chama chake.

"Naomba kutoa taarifa kwa umma wa Watanzania kuwa leo (jana) nimeandika barua kwenda kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kujiuzulu nafasi ya Spika wa Bunge," alisema Ndugai.

"Nakala ya barua yangu hiyo ya kujiuzulu nimeiwasilisha kwa Katibu wa Bunge kwa ajili ya hatua stahili kwa mujibu wa Katiba ya nchi na sheria zingine husika ili kuwezesha mchakato wa kumpata Spika mwingine kuanza," aliongeza na kuongeza kuwa:

"Nachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wabunge wenzangu, Rais Samia Suluhu Hassan, serikali kwa ujumla, wananchi wa jimbo langu la Kongwa na Watanzania wote kwa ushirikiano mkubwa mlionipa katika kipping chote nilipokuwa Spika wa Bunge letu tukufu," alisema.

**KATIBA INASEMAJE**

Kwa mujibu wa Ibara ya 84 (7) (a-h), Spika atakoma kuwa Spika na ataachia kiti cha Spika litokeapo iwapo, mosi, mtu huyo atachaguliwa kutoka miongoni mwa wabunge, basi ikiwa atakoma kuwa Mbunge kwa sababu yoyote ambayo haihusiki na kuvunjwa Bunge au ikiwa kutatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Spika, lisingemfanya mtu huyu asiwe na sifa za uchaguzi au apoteze sifa za uchaguzi wa Spika.

Pili; Bunge litakapokutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu uliofanywa baada ya Bunge kuvunjwa, lakini masharti ya aya hii yatatumika bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (4) ya ibara ya 90 ya Katiba.

Tatu, ikiwa mtu huyo ataondolewa kwenye madaraka ya Spika kwa azimio la Bunge liliungwa mkono na wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya wabunge wote na nne, ikiwa mtu huyo atashindwa kuwasilisha kwa Rais tamko rasmi kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo (5) ya ibara hii.

Tano, ikiwa mtu huyo atapatikana na hatia kwa kosa la kutoa habari za uongo kwa kiapo kinyume cha sheria ya kanuni ya jinai, kuhusu tamko rasmi lolote lililotolewa kwa mujibu wa msharti ya ibara ndogo ya (3) ya ibara hii.

Ikiwa mtu huyo atashindwa kuwasilisha kwa Rais taarifa ya mali kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (5) ya ibara hii kabla ya kumalizika muda uliowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Ikiwa itathibitika mtu huyo amevunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Aidha, ibara ndogo ya 8 inasema "Hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge isipokuwa uchaguzi wa Spika wakati wowote ambao kiti cha Spika kitakuwa ki wazi.

Pia inaeleza kuwa mtu yeyote ambaye si Mbunge atakayechaguliwa kuwa Spika atatakiwa, kabla ya kuanza kutekeleza madaraka yake kuapishwa katika Bunge kiapo cha uaminifu.

**WAKILI AFUNGUKA**

Wakili wa kujitegemea John Mallya, kuhusu Katiba kuwa kimya alisema: "Kuna 'lacuna' (upungufu) wa kisheria kitu gani kifanyike na hii inadhihirisha waliotunga mwaka 1977 hawakuona kwamba kuna siku kiongozi wa muhimili atajiuzulu. Hii inaonyesha tunahitaji mabadiliko na lazima tuwe na Katiba inayobeba mazingira yote."

Kwa mujibu wa Mallya, Bunge lina upungufu wa kimuundo na utendaji kwa kuwa mabunge yote nchi za Jumuiya ya Madola kama Kenya, Uganda na Uingereza muda wote bunge linaendelea hakuna vipindi kama kwetu maana yake kama Katiba haijasema lolote inapotokea amejiudhulu wabunge wanamchagua Spika mwingine kwa haraka.

"Mfano Rais alivyofariki dunia ingekuwa muda ambao si wabunge maana yake Rais Samia angeteua Makamu wa Rais na kuita bunge la dharura jambo ambalo kwingine haliko hivyo," alisema.

**LHRC**

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema kilichofanywa na Ndugai ni uwajibikaji kwa kuwa ameona kosa lake la kudhalilisha muhimili anauongoza na mwingine jambo linalolegeza nchi.

"Kilichonishtua si nchi kuuzwa bali kulalamika wakati yeye ni muhimili, ameona amekosea kaomba msamaha na kuamua kujiuzulu,"alisema.

Kuhusu ukimya wa Katiba, alisema "Tuna upungufu wa wa Katiba kilipaswa kuwepo kifungu kinachoeleza iwapo atajiudhulu. Hii inaonyesha umuhimu wa Katiba Mpya kwa kuwa walitunga hawakutegemea kuwa ipo siku Spika au kiongozi mwingine atajiudhulu, kuna haja ya kuwa na katiba inayoeleza iwapo Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika na Jaji Mkuu watajiuzulu nini kitatokea," alifafanua.

**JUKATA**

Mjumbe wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda, alisema, kutokana na uamuzi wa Spika Ndugai kujiuzulu, ni wakati wa Tanzania kupata Katiba mpya, ambayo itabainisha wazi nguvu ya mihimili mitatu.

Mwakagenda, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD), alisema: "Mihimili haipo yote, isipokuwa mmoja tu. Spika, ambaye ni mhimili wa bunge hawezi kutolewa kirahisi.

"Hoja aliyoitoa ingejengwa kama hoja, na ni maoni yake. Hii inatuthibitishia kwamba ni wakati wa kupata katiba mpya ambayo italinda kila mhimili."

■ **Imeandikwa na Salome Kitomari, Gwamaka Alipipi na Christina Mwakangale**

**HABARI KITAIFA**

# Anusurika kuchomwa moto madai ugoni

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKAZI wa Chamwino, Manispaa ya Morogoro, Daudi Emanuel (27) amenusurika kifo baada ya kumwagiwa mafuta ya petroli kisha kuchomwa moto na rafiki yake, Marko Gerald, baada ya kumtuhumu kuwa amembaka mke wake.

Akisimulia madhila yaliyomkuta huku akiugulia maumivu makali wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Emanuel alisema tukio hilo lilitokea Januari 2, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku.

Siku ya tukio, alisema rafiki yake alimwita nyumbani kwake ili kumsaidia kushusha na kupanga magunia ya mkaa na baadaye aliondoka na kumwacha na mkewe wakiwa wanamsubiri ili waendelee na kazi aliyomwitia.

Alisema baada ya rafiki yake kuondoka, shemeji yake alikwenda kuoga na alipotaka kubadili nguo aliondoka kwa lengo la kumpisha ili avae ndipo rafiki yake huyo akarejea na kukuta mkewe akiwa anavaa, hivyo kuhisi amefanya naye tendo la ngono.

"Mimi nilitoka nje kumpisha shemeji avae nguo zake, sasa yeye aliporudi na kumkuta mke wake ametoka kuoga ndipo akaanza kuhisi vibaya. Alivyoona mimi sipo akanipigia simu niende alipo na nilipofika nikamkuta akiwa na watu watatu wakanikamata na kunipeleka kwenye boma (nyumba ambayo haijaisha) na kunifanyia kitendo hiki," alisema Emanuel.

Amina Shomari, Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, alisema majeruhi huyo alipokewa Januari 3, akiwa ameungua sehemu ya juu ya ngozi katika sehemu kubwa ya mwili wake.

Shomari alisema kwa sasa hali yake inaendelea vizuri baada ya kupata matibabu ikiwamo kufunga vidonda vyake kwa kusafisha na dawa ambazo zitaweza kurejesha ngozi yake na kupona majeraha hayo.

"Hali yake inaendelea vizuri kwa sasa baada ya kupata matibabu na dawa ambazo anaendelea kutumia. Kwa hali inavyoendelea, tunaamini ataendelea kupata matibabu hapa hapa mpaka atakapopona kabisa," amesema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fortunatus Musilimu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba tayari watu wawili wanashikiliwa kwa tuhuma za kuhusika na kitendo hicho.

Aliwataja waliokamatwa kuwa ni Marko Gerard (28) na mke wake ambaye jina lake linahifadhiwa.

"Huyu Marko tayari tumeshamkamata lakini alishirikiana na watu watatu ambao wametoroka baada ya kufanya tukio hilo ambalo chanzo chake ni huyu Marko kumtuhumu Daudi kuwa amembaka mkewe ambaye naye tunamshikilia. Hao wengine tunaendelea kuwatafuta kwa hatua zaidi za kisheria," alisema.



Abiria wakiwa katika kituo kikuu cha mabasi mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana, kwa ajili ya kurudi katika mikoa mbalimbali nchini, baada ya kumalizika kwa mapumziko ya sikukuu za mwisho wa mwaka. Baadhi yao wamelalamikia kitendo cha wenye mabasi kupandisha nauli kutokana na wingi wa abiria. **PICHA: MARY MOSHA**

# Shahidi adai washtakiwa walikiri kuwapo kupokea rushwa mil. 90/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHAHIDI wa 13 upande wa Jamhuri ameiambia Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, kuwa washtakiwa wenzake, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Lengai Ole Sabaya baada ya kukamatwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), walikiri kuhusika katika tukio la uporaji fedha Sh. milioni 90 za Mroso Januari 22, 2021.

Washtakiwa wengine mbali na Sabaya ni Enock Togolani, Watson Mwahomange, Sylivester Nyegu, John Odemba, Jakson Macha na Nathan Msuya.

Alidai hayo jana mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda, wakati akihojiwa na wakili wa utetezi Mosses Mahuna. Ramadhani alidai kuwa baada ya kukamatwa washtakiwa hao, hakuona haja ya kufanya gwaride la utambulisho kwa sababu maelezo aliyopata kwa Francis Mroso, uchunguzi wake haukuwa na mashaka kama washtakiwa hao hawahusiki na walikiri kuhusika.

Sehemu ya mahojiano hayo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Wakili:** Unahakika gani siku ya tukio Sabaya alikuwa Arusha?

**Shahidi:** Ninahakika kupitia taarifa za Vodacom

**Wakili:** Unahakika gani siku hiyo walikuwa na simu hiyo.

**Shahidi:** Kweli siku ya Januari 22, mwaka 2021 alikuwa na simu zake na mtandao wake wa kihalifu.

**Wakili:** Ni kweli ulikamata hawa wote hakuna gwaride la utambulisho ili Mroso atambue waliofika kwenye gereji yake?

**Shahidi:** Kweli hakuna gwaride lililofanyika.

**Wakili:** We ulifanya mahojiano na Sabaya akawataja ili uwakamate?

**Shahidi:** Sijawahi.

**Wakili:** Mroso katika maelezo yake polisi alitaja watu warefu wenye misuli, sura pana na maumbile ya kutisha ndio hawa aliwataja?

**Shahidi:** Ndiyo

**Wakili:** Uliwakamata kwa sababu gani?

**Shahidi:** Niliwakamata kupitia maelezo ya Mroso na uchunguzi mbalimbali nilioufanya.

**Wakili:** Mashtaka haya makubwa hukuona umuhimu wa kuitisha gwaride la utambuzi?

**Shahidi:** Sikuwa na mashaka sababu baada ya kukamatwa walikiri kuwa miongoni mwao.

**Wakili:** Zipo wapi 'Statement' zao za kukiri?

**Shahidi:** Zitaletwa zikihitajika

**Wakili:** Kosa la Mroso lilikuwa nini hadi aambiwe atoe Sh. milioni 90?

**Shahidi:** Kutokutoa risiti za kielektroniki (EFDs)

**Wakili:** Una hakika siku ya Januari 20, 2021 hakutoa risiti?

**Shahidi:** Ndiyo hakutoa.

**Wakili:** Je, kutokutoa risiti za EFDs ni kosa?

**Shahidi:** Ndiyo ni kosa.

**Wakili:** Je, ni kosa la uhujumu uchumi?

**Shahidi:** Wenye kulisemea hilo ni TRA.

**Wakili:** Je, Mroso aliwahi kukufahamisha alimwambia meneja wa tawi kuwa anatoa Sh. milioni 90 kuwa anaenda kulipa deni?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Wakili:** Je, hakuwahi kusema kwa Meneja wa tawi kuwa anachukua fedha hizo sababu amelazimishwa na Sabaya?

**Shahidi:** Ndiyo hakuwahi kusema hayo.

**Wakili:** Je, ni kweli katika uchunguzi wako umebaini Mroso alibeba boksi la Sh. milioni 90 na kwenda nalo kwenye gari akaweka kiti cha mbele?

**Shahidi:** Ni kweli Mroso alibeba fedha na gari lilikuwa la Mroso.

**Wakili:** Nani alishusha pesa kuitoka kwenye gari.

**Shahidi:** Johson Macha ambaye alikuwa kwenye gari kutoka benki na nilibaini kupitia uchunguzi na mahojiano na shahidi.

**Wakili:** Pesa za nani na gari la nani?

**Shahidi:** Ndio zilikuwa za Mroso na gari la Mroso.

**Wakili:** Rushwa ilitolewa wapi na saa ngapi?

**Shahidi:** Ilitolewa katika gari.

**Wakili:** Nini kinakufanya useme rushwa wakati pesa zilichukuliwa kwenye gari?

**Shahidi:** Mazingira yote yaliyokuwapo na ushawishi na zipo simu nyingi alizokuwa akiongea naye Mroso.

**Wakili:** Una ushahidi mwingine ulioleta mahakamani?

**Shahidi:** Sijaleta.

**Wakili:** Baada ya kupokea pesa hizo, Lengai alienda Tulia Hotel na alikilipia?

**Shahidi:** Ndio alichukua vyumba na kuvilipia.

**Wakili:** Je, fedha hizo umeleta hapa mahakamani kama ndizo zilizoibiwa kwa Mroso?

**Shahidi:** Sijaulizwa.

**Wakili:** Mroso amewahi tambua fedha zilizoibiwa.

**Shahidi:** Fedha ni mali ya serikali.

**Wakili:** Katika ushahidi wako umesema Lengai kama mtumishi wa umma asingeweza nunua gari lile V8 ya Sh. milioni 60 wakati alikuwa mkuu wa wilaya mwenye akili.

**Shahidi:** Nimesema aina ya maisha aliyokuwa anaishi hakuwa na biashara yoyote na katika uchunguzi wangu nimebaini hilo, hivyo ngumu kuwa na fedha za kununua gari hilo.

**Wakili:** Hujui Sabaya ni Mmasai ana mifugo?

**Shahidi:** Hana mifugo yoyote.

**Wakili:** Kwanini vielezo vyote unavyozungumza hapa hukuvileta ni sahihi mnaficha baadhi ya vielelezo na mmeleta vile tu mnavyotaka nyie?

**Shahidi:** Sio kazi yangu kuamua nilete kielelezo gani hapa.

**Wakili:** Hayo maelezo ya kukiri ambayo hukuyaleta hapa yalikuwa ya lini?

**Shahidi:** Maelezo yao ya Jakson Macha, Nathan Msuya nilichukua Juni 17, 2021 baada ya kuwakamata Juni 15, mwaka 2021.

## HABARI KITAIFA

# Wanafunzi milioni 3.8 kujiunga shule nchini

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesema ujumla ya wanafunzi milioni 3.8 watajiunga na darasa la awali, la kwanza na kidato cha kwanza nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, alisema wanafunzi wote wataendelea na masomo bila tatizo kutokana na kwamba asilimia 95 ya vyumba vya madarasa vimekamilika katika maeneo mbalimbali nchini.

Alibainisha kuwa darasa la awali ni milioni 1.3, darasa la kwanza milioni 1.5 na kidato cha kwanza 907,803, na kwamba ongezeko la wanafunzi limeongeza mahitaji ya miundombinu kama madarasa, nyumba za walimu, matundu ya vyoo, maabara na maktaba.

"Ni dhahiri kuwa hali ya uandikishaji wa wanafunzi hauridhishi, darasa la awali ni mkoa mmoja ndio wenye uandikishaji wa angalau asilimia 50, mikoa 25 ya Tanzania Bara bado ina uandikishaji chini ya asilimia 50," alibainisha Ummy.

Aliongeza kuwa kwa darasa la kwanza mikoa ambayo imeandikisha zaidi ya asilimia 50 ni tisa, huku mikoa 17 ikiwa chini ya asilimia 50 na kwamba zaidi ya asilimia 80 ya wanafunzi wa darasa la awali wameandikishwa shule za serikali.

Kwa mujibu wa Ummy, mikoa iliyoongoza kwa uandikishaji na asilimia zake kwenye mabano ni Manyara (57.9), Mara (49.3), Njombe (49), Tanga (47.8) na Mbeya (46.99).

Mingine ambayo takwimu iko chini na asilimia zao kwenye mabano ni Mwanza (21), Dar es Salaam (20), Mtwara (19.5), Rukwa (17) na Katavi (8.93).

"Nimepokea taarifa kwamba kuna baadhi ya wakuu wa shule wanatoza michango kwa ajili ya uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali na la kwanza, na inawezekana ndio sababu ya kuwa na uandikishaji mdogo wa wanafunzi katika shule zetu. "Wakuu wa shule hatutasita kuwachukulia hatua kali yoyote ambaye tutam'baini anakiuka maelekezo haya ya serikali, lakini maofisa elimu wa wilaya na mikoa watawajibika kwa suala lolote ambalo tutalibaini kuwa shule yoyote zilizo katika wilaya, mikoa yao zinatoza michango kwa ajili ya kuandikisha wanafunzi," alisema Ummy.

Alieleza kuwa ili waweze kupeleka kiwango sahihi cha fedha za elimu bila malipo wanahitaji suala la uandikishaji lifikie asilimia 90, katika shule za msingi na sekondari, akidai kuwa kama shule itakuwa imeandikisha wanafunzi 1,000 wakati inatakiwa wanafunzi 10,000 watapatiwa fedha za wanafunzi 1,000.

Katika kuhakikisha suala hilo linafanikiwa aliitaka mikoa kuweka utaratibu kwa viongozi walioko katika ngazi ya tarafa, kata, vijiji, mitaa na vitongoji, ili waweze kupita kila sehemu kuhimiza watoto wote wenye umri wa kuandikishwa awali na darasa la kwanza wanafanya hivyo mara moja. "Mikoa itaweka mikakati yao kama ni magari ya matangazo yatapita kijiji kwa kijiji, mtaa kwa mtaa, nyumba kwa nyumba, na ninaitaka mikoa isisite kuwachukulia hatua wazazi/walezi ambao wanawaficha watoto wenye umri wa kwenda shule, ni lazima wawachukulie hatua kali kwa mujibu wa sheria na taratibu," aliagiza Ummy.

Pia alitoa wito kwa wakuu wa mikoa kuhakikisha wanafunzi wote walioacha shule kwa sababu mbalimbali, ikiwamo ujauzito wanarejea shuleni kwa kuzingatia miongozo ya elimu ikiwa ni pamoja na waraka wa elimu namba tatu wa mwaka 2021 na maelekezo ya Baraza la Mitihani Tanzania.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa maelekezo kwa wakuu wa shule za serikali kutowatoza ada wazazi wanaotaka kuwaandikisha watoto shule. Kushoto ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Gerald Mweli. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uokozi boti iliyozama wasitishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAZI ya uokoaji katika ajali ya boti Kisiwa Panza kisiwani Pemba imesitishwa baada ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kujiridhisha kuwa hakuna taarifa za mtu ambaye alipanda katika boti hiyo na haonekani.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa KMKM, Luteni Sharif Mshenga, alisema licha ya kusitisha kazi hiyo katika eneo la tukio, wanaendelea kufanya doria katika maeneo mengine nje ya eneo la ajali.

Mshenga alisema kazi hiyo ilisitishwa juzi majira ya saa 12:00 jioni baada ya kujiridhisha na taarifa kutoka kwa masheha zikiwamo shehia za Kisiwa Panza, Makoongo na Chokocho kuwa hakuna taarifa za mtu ambaye jamaa yake haonekani baada ya ajali hiyo.

"Tumefanya udadisi kwa mashekha na wananchi kama kuna mtu yeyote ambaye haonekani ili kupata taarifa zake, lakini hakuna taarifa, hivyo tunaendelea na operesheni ndogo ndogo baharini ili kujiridhisha," alisema Luteni Mshenga. Alisema hakuna taarifa rasmi ya idadi ya watu waliokuwa wanasafiri katika boti hiyo aina ya Ngwanda itawayo Kiromoko na kwamba waliokolewa wakiwa hai ni 15 na waliofariki dunia ni 10.

Kamanda huyo alisema kitaalamu mtu anapozama chini ya bahari huwa hazizidi saa 48 mwili utaibuka juu na kuelea juu ya bahari au kusombwa na maji.

"Kwa kweli tuna masikitiko makubwa kwa tukio hili lililotokea Januari 4 la kuzama kwa chombo cha usafiri baharini. Lakini tunawasihi wananchi kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu cha msiba," alisema Luteni Mshenga.

Mshenga pia aliwataka wananchi wa visiwani kutumia vyombo vya usafiri baharini vilivyotambuliwa na serikali ambavyo vina usalama zaidi hasa inapotokea ajali zikiwamo zana za uokoaji.

Alisema mwishoni mwa mwaka jana, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alizindua boti ndogo za usafiri wa abiria kwa visiwa vidogo vya Makoongwe na Kisiwa Panda lakini baadhi ya watu hawazitumii.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, sababu za kutozitumia boti hizo ni madai kuwa zinafunga gati katika Bandari ya Mkoani, hivyo kuvifuata eneo hilo ni masafa marefu.

"Niwaombe wananchi kuvitumia vivuko hivi vilivyotolewa na serikali kwa ajili ya usalama wao," alisisitiza.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Pemba, Khatib Juma Mjaja, aliwataka wananchi hasa wavuvi, kutoa taarifa katika sehemu husika iwapo watakuta mwili ukielea au ukiwa pembezoni mwa bahari ili kujiridhisha kama unatokana na ajali hiyo.

Ajali ya kuzama kwa boti hiyo ilitokea Januari 4, mwaka huu, majira ya saa 10:00 jioni wakati zaidi ya watu zaidi ya 20 waliokuwa wakisafiri kwa ajili ya kwenda msibani wakitokea Chakechake kwenda Kisiwa Panza Mkoa wa Kusini Pemba.

# Makalla atoa neno vinara mgogoro wa ardhi Mabwepande

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amepokea ripoti ya kamati aliyounda kuchunguza migogoro sugu ya ardhi eneo la Mabwepande ambayo ina mapendekezo 19 ya kufanyia kazi kumaliza migogoro hiyo.

Baada ya kupokea ripoti hiyo juzi, Makalla aliikabidhi kwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, na Mkurugenzi wa Manispaa na kuwaelekeza kuitisha kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ili kupitia ripoti na kutekeleza mapendekezo hayo.

Pia alielekeza vyombo vya dola kuwakamata watu wote waliobainishwa na kamati kuwa vinara wa kusababisha migogoro na kuwachukulia hatua za kisheria.

Licha ya kuikabidhi kwa mkuu wa wilaya, Makalla alisema ripoti hiyo ataikabidhi kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi huku akibainisha kuwa watuhumiwa wote ambao wako chini ya mamlaka ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wafikishwe kwenye kamati ya maadili na kuchukukiwa hatua.

Makalla alimwelekeza Gondwe kumpatia mpango kazi wa kutekeleza mapendekezo yote 19 ya kamati. Aliipongeza kamati kwa kazi kubwa na nzuri iliyofanya.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Siraji Ngarambe, alisema kamati hiyo ilifanya kazi kwa siku 78 na kubaini miongoni mwa sababu za migogoro waliyobaini kuwa ni pamoja na watendaji wa kata, mitaa, wajumbe wa shina wasio waaminifu, ugawaji wa maeneo pasipo kufuata taratibu, rushwa, matumizi mabaya ya kauli za viongozi na dhana iliyojengeka kwa baadhi ya wananchi kuvamia maeneo ili walipwe fidia.

## TANGAZO

# MINIMUM DISCLOSURE OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

NMB
Close to you

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNTS** | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Pamoja A/C TZS 30,000 |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 ; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| 2 | **CURRENT ACCOUNT** | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C & Agribusiness - TZS 15,340; Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is - TZS 1,800; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| 3 | **EFT** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| 4 | **TISS** | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT | Savings Acc | Current Acc |
|---|---|---|---|
| | Transaction fee | N/A | N/A |
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |
| 6 | **ATM CARD AND TRANSACTIONS RELATED** | | |
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 5,900 ; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800 ; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800 ; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |
| 7 | **MOBILE (SMS) BANKING** | | |
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 400 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | FREE |
| 8 | **INTERNET BANKING** | | |
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |
| 9 | **MONEY REMITTANCES** | | |
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |

| 10 | BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES | | |
|---|---|---|---|
| A | TYPES OF LENDING RATES | LENDING RATES - PA (%) | |
| | | TZS | USD |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 15% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

**B FIXED DEPOSITS**

| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Saving account rates up to 12%**

**Signed By:** **Aloyse Maro, Head Retail Products & Channels** — **Filbert Mponzi, Chief Retail Banking**




www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunatarajia kasi uunganishaji umeme

**SHIRIKA** la Umeme Tanzania (TANESCO), limetangaza kurudisha gharama za awali za kuunganisha huduma ya umeme kwa wateja wake, kama zilivyokuwa zimetangazwa kwenye gazeti la serikali mwaka jana.

Gharama hizo zilitangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA), kwenye gazeti la serikali namba 1020 Desemba 4, mwaka jana, na imefafanuliwa kuwa gharama zote zimejumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa gharama hizo ziliidhinishwa rasmi na EWURA Novemba 25, mwaka jana, baada ya kupitia mchakato wa tathmini wa bei kulingana na gharama halisi ya vifaa vya uunganishaji umeme na kwamba kwa sasa itaondoa kero ya kushindwa kuwafungia huduma ya umeme wateja wake kwa wakati.

Kuanzia sasa gharama za kuunganisha umeme mjini ndani ya mita 30 kwa mteja wa njia moja kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 320,960, kwa mteja wa njia moja ndani ya mita 70 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 515,618 na kwa umbali wa njia moja ndani ya mita 120 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 696,670.

Pia gharama za kuunganisha umeme mjini ndani ya mita 30 kwa mteja wa njia tatu kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 912,014, kwa mteja wa njia tatu ndani ya mita 70 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 1,249,385, umbali wa njia tatu ndani ya mita 120 kutoka kwenye miundombinu ya umeme ni Sh. 1,639,156.

TANESCO imesema gharama ya kuunganisha umeme vijijini kwa wateja wa njia moja ni Sh. 27,000 kama ilivyoelekezwa na EWURA.

Pia wateja waliokwisha lipia Sh. 27,000 kwa ajili ya kuunganishiwa huduma hiyo, wanatakiwa kufika ofisi za shirika hilo.

TANESCO ilipata nguvu ya kutekeleza bei hizo baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kusema wazi kuwa bei ya kuunganishia watu umeme kwa sasa haina uhalisia, kiasi cha wengi kushindwa kupata huduma hiyo.

Alisema bayana kuwa gharama hizo ndogo zilisababisha shirika hilo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kuunganishia watu umeme, na kuagiza wasiweke viwango vya juu sana bali halisia.

Katika hili kuna jambo kubwa la kujifunza kwamba wakati mwingine watendaji wanashindwa kushauri au kusema uhalisia wa uendeshaji kwa kuwa kiongozi mkuu ndiye aliyeamua, matokeo yake mashirika yanaumia yenyewe na wananchi wanashindwa kupata huduma sahihi.

Ni muhimu viongozi wakuu wanapofanya uamuzi kabla ya kutangaza kwa umma wawe wametafakari kwa kina, ikiwamo kupokea ushauri ili kuepusha kuyaumiza mashirika na taasisi zake au kuwaweka kwenye wakati mgumu watendaji wake kama tunavyoona kwa TANESCO.

Sasa TANESCO wamepewa rungu na bei halisi zitatumika kuunganishia wananchi umeme, tunatarajia kuona kasi ya kuwahudumia wateja ambao watalipa ili kuondoa usumbufu au kukaribisha mazingira ya rushwa.

Tunatarajia kuona mabadiliko na kasi ya kuhudumia wateja ili kufungiwa umeme isiwe anasa bali haki ya Mtanzania ambaye ameshalipia huduma hiyo kwa mujibu wa sheria na sio kukwamisha hadi uwe unafahamiana na mtu au kutoa kitu kidogo.

Miaka ya nyuma kupata huduma TANESCO ilikuwa ngumu mpaka ufahamiane na mtu, ndiyo ufungiwe huduma hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamani tuwe na subira, kukamilika miradi hii itaipa tija uchumi wetu

Na Rajabu Msangi -SJMC

**DHANA** ya ukuaji uchumi inaweza kuzua kitendawili kwa viongozi wa serikali na hata wananchi wa chini, ndani ya lengo lake la kutaka maendeleo katika taifa. Nikitazama miradi ya kimkakati inayofanywa na serikali naona ina tija kubwa kitaifa, huku ikisadikika kukuza uchumi wa taifa, kuzalisha ajira kwa vijana na kupunguza madeni tunayodaiwa.

Nchi yetu Tanzania ilibahatika kupandishwa daraja la kufikia uchumi wa kati, mwaka 2020 na Benki ya Dunia. Ni wazi kuwa nchi nyingi duniani ziliteteteka kiuchumi wakati wa janga la virusi vya corona, ambavyo bado ni tishio duniani katika wimbi hili la sita.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, ameshuhudia hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Makutupora - Tabora, kinachotarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. trilioni nne.

Katika hafla hiyo, Rais Samia alieleza umuhimu wa kukamilisha miradi hiyo katika kukuza uchumi wa taifa letu.

"Mimi nipo pamoja nanyi, tutaangalia mikopo inayotufaa, tukiongozwa na Gavana wa Benki Kuu (BOT) na waziri yupo hapa, tutachukua tumalize reli kama tulivyopanga ili ifanye kazi, itengeneze fedha tuweze kulipa mikopo tunayoichukua," alitamka.

Kukamilika miradi hiyo kunaonyesha taswira halisi ya kuja kuzalisha ajira kwa vijana, pia kuongeza pato nchini hasa katika ulipaji kodi. Nchi yetu ina miradi mingi inayopaswa kukamilika na bado serikali inajitahidi kuhakikisha inakamilisha miradi hiyo.

Wakati ambao Watanzania tunapaswa kuwa wamoja ni huu, kwa kushikamana na Rais Samia katika kutekeleza shughuli za maendeleo ya nchi yetu.

**Haya nayathibitisha pale Rais aliposema katika miradi hii ya kimkakati, wapo baadhi ya watu waliokuwa wanasubiri kuona miradi hiyo inakwama, ili wapate la kuzungumza, lakini Rais alisisitiza hakuna utakaokwama.**

Haya nayathibitisha pale Rais aliposema katika miradi hii ya kimkakati, wapo baadhi ya watu waliokuwa wanasubiri kuona miradi hiyo inakwama, ili wapate la kuzungumza, lakini Rais alisisitiza hakuna utakaokwama.

Alitamka: "Kuna mradi wa Bwawa la Nyerere, Daraja la Busisi, sijui miradi ya barabara, sijui reli na mingine yote, hakuna hata mmoja ambao tunadaiwa pesa, makandarasi wameshalipwa yote, sisi ndio tumebaki tunadai kazi".

Kauli ya Wahenga ya 'umoja ni nguvu Utengano ni udhaifu' tunapaswa kuishi nayo Watanzania katika kuhakikisha lengo letu la kukamilisha miradi hii linafikia suluhisho bora.

Mradi huu wa SGR utakuwa na faida lukuki si kwa Tanzania pekee hata katika maendeleo ya Afrika. Wakati Rais Samia alipoweka jiwe la msingi la ujenzi huu kutoka Mwanza hadi Isaka mwezi Juni mwaka huu, alieleza moja ya umuhimu wa miradi huu.

"Moja ya mambo yanayotajwa kukwamisha kasi ya maendeleo Afrika ni kutokuwapo miundombinu imara ya usafiri. Utafiti unaonyesha kuwa ukosefu na ubovu wa miundombinu sio tu unachelewesha usafirishaji wa watu na bidhaa, bali unaongeza gharama za bidhaa kwa asilimia 40," alisema Rais Samia.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania, Masanja Kadogosa, anasema ujenzi kutoka Mwanza kwenda Isaka utawazalishia Watanzania ajira zaidi ya 86,000.

Ni faida lukuki kukamilika kwa miradi yote ya kimkakati kutawezesha kupunguza gharama na usumbufu kwa wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kutoka nje ya nchi na kulazimika kusafiri hadi mkoani Dar es Salaam kupokea mizigo yao.

Tukiishi na imani kwa viongozi wetu wa serikali, tukishikamana wananchi kwa umoja, tutaweza kufanikisha zoezi letu la kufikia malengo ya maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania.

## ...Alikotoka Job Yustino Ndugai

**Na Mwandishi Wetu**

JOB Yustino Ndugai, alizaliwa Januari 21, 1963 Kongwa mkoani Dodoma na aliingia katika Bunge la Tanzania baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kielimu, Ndugai ni msomi mwenye shahada tatu, ikiwamo ya kwanza na mbili za umahiri katika masuala ya sayansi na uongozi wa biashara alizozipata katika vyuo vikuu ndani na nje ya nchi.

Safari yake ya elimu ilianzia katika Shule ya Msingi Matare, Kongwa mwaka 1971 hadi 1977 na baadaye kujiunga na elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari ya Kibaha mkoani Pwani kuanzia mwaka 1978 hadi 1981 kidato cha kwanza hadi cha nne. Baada ya hapo alijiunga na Shule ya Sekondari ya Old Moshi kwa masomo ya kidato cha tano na cha sita mwaka 1982 hadi 1984.

Mwaka 1989 alichaguliwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa shahada ya kwanza katika sayansi aliyohitimu mwaka 1993. Mwaka 1994 alijiunga na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway na kutunukiwa shahada ya Umahiri katika sayansi ambako alihitimu mwaka 1996.

Licha ya kuhitimu shahada hizo za sayansi na kufanya kazi katika masuala ya uhifadhi hadi alipoingia katika ubunge mwaka 2000, Ndugai pia alijiunga na Chuo Kikuu cha Maastricht, Uholanzi na kuhitimu shahada ya umahiri katika uongozi wa biashara (MBA).

Mbali na shahada hizo, Ndugai pia alihudhuria kozi mbalimbali za uongozi zikiwamo za mafunzo ya kompyuta (2000), Uongozi nchini Ireland (2003), Chuo Kikuu cha New York, Marekani (2009) na Nairobi, Kenya (2011). Kozi nyingine ni uongozi wa Bunge (Parliamentary Leadership), Dubai mwaka 2013.

UBUNGE NA UONGOZI

Ndugai hadi sasa amekuwa Mbunge wa Kongwa tangu mwaka 2000 baada ya kuacha kazi katika Wizara ya Maliasili na Utalii ambako alishika nyadhifa mbalimbali hadi kufikia nafasi ya meneja.

Baada ya kuingia Bungeni, alikuwa mmoja wa wabunge machachari waliokuwa wakiuliza maswali hata kuibana serikali juu ya masuala mbalimbali, hatua hiyo ilimfanya atajwe kuwa mbunge machachari katika Bunge la tisa.

Mwaka 2005 alioshinda tena ubunge katika Jimbo la Kongwa. Nyota yake ilianza kung'ara zaidi baada ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi na Mazingira, nafasi iliyomfanya kuwa Mwenyekiti wa Bunge, akiongoza vikao vya Bunge kama Spika na naibu wake hawapo. Kimo chake kilikuwa kikiwafanya wabunge kupiga kofi kila alipokuwa akikalia kitu kuongoza vikao.

Ndugai alirejea bungeni kwa mara ya tatu mwaka 2010 na hatimaye alichaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge chini ya Anne Makinda ambaye kabla ya hapo alikuwa naibu spika.

Mwaka 2015 baada ya uchaguzi mkuu uliomwingiza John Magufuli kuwa Rais wa awamu ya tano, Ndugai alichaguliwa kuwa Spika wa Bunge katika uchaguzi wa Spika uliofanyika Novemba 17, 2015. Alishinda nafasi hiyo kwa kupata kura 254 kati ya 354 za wabunge wote akimshinda aliyekuwa mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Goodluuck ole Medeye aliyepata kura 109.

Kutokana na wadhifa wa Spika, Ndugai amekuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) na Kamati Kuu ya Jalmashauri Kuu ya Taifa (CC- NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

# Kila kona walitaka Ndugai ajiuzulu

**Na Elizabeth Zaya**

KABLA ya kutangaza uamuzi wa kujiuzulu, Mabaraza ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) kutoka mikoa mbalimbali nchini pamoja na baadhi ya wanasiasa wa chama hicho, walimtaka Spika wa Bunge, Job Ndugai kujiuzulu nafasi yake hiyo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, walisema kauli aliyoitoa Spika ni ya usaliti ndani ya chama ya kumdhalilisha Rais ambaye ni Mwenyekiti wa chama hicho na imeleta taharuki si ndani ya chama hicho bali kwa Watanzania wote.

Mwenyekiti wa UVVCCM Mkoa wa Mtwara, Nasibu Kanduru, alisema pamoja na Ndugai kuheshimiwa na chama hicho kwa kupitisha jina lake kwenda kukiwakilisha katika mhimili wa Bunge, lakini yeye amekidhalilisha na amekishusha hadhi.

"Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia mhimili wa Bunge kilipitisha jina la Ndugai kwenda kukiwakilisha kama Spika wa Bunge na kilimpitisha kwa kura za kishindo, ilikuwa heshima kubwa ambayo chama chetu kilimkabidhi. Lakini ndani ya wiki moja Ndugai aliongea kauli ambazo taifa letu limekuwa katika taharuki kubwa sana. Aliongea kauli ambazo, zinamdhalilisha Rais, lakini zinazoshusha heshima ya CCM, sisi kama UVCCM mkoa wa Mtwara tumekwazika."

Alisema nafasi aliyonayo Spika kwenye chama alikuwa na uwezo wa kuomba kuonana na Rais, kumpigia simu au kumwandikia barua ya kuomba ufafanuzi na pia alikuwa na fursa nyingi za kiserikali na kupitia muhimili anaouongoza, lakini hakutaka kuzitumia zote.

**UVCCM NJOMBE**

"Sisi Umoja wa Vijana Mkoa wa Njombe tunaamini kuwa Ndugai anapaswa kulinda heshima ya bunge letu tukufu la JMT. Kutokana na kauli zake tunamwomba akae pembeni kulinda heshima ya bunge letu," alisema Nehemia Mtweve, Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa huo.

**MAKALLA ANENA**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema, kauli ya Ndugai kwamba nchi inaweza ikauzwa kutokana na madeni ilisababisha aingie kwenye mitandao na kuanza kutafuta kama kuna nchi duniani iliyowahi kuuzwa kutokana na madeni.

"Niliposikia kwamba nchi yetu inaweza kuuzwa kwa mnada, nataka niwahakikishie nimejiridhisha, hakujawahi kutokea nchi duniani ikauzwa. Ilinilazimu mimi kwenda kugoogle (kutafuta kwenye mitandao) nimetafuta mara tatu, zinanikatalia, niligoogle (nilitafuta) mfano wa nchi iliyouzwa, ikanionyesha kwamba zijue haki tano za mtoto," alisema Makalla.



**UVCCM KILIMANJARO**

UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro ulimtaka Ndugai kujiuzulu ili kulinda haki na heshima yake na bunge.

"Waswahili husema "msiba wa kujitakia hauna kilio" hivyo fitina na unafiki wa spika Ndugai unamwajibisha mwenyewe, msingi wa hoja hii ni undumilakuwili wake, ambaye hapo awali alipongeza mikopo hii na baadaye kupinga vikali. Hapa inaonekana wazi tatizo sio mkopo, bali ana lake."

**UVCCM DAR ES SALAAM**

Umoja wa Vijana wa chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam, walimtaka Ndugai kujiuzuru na kukabidhi ofisi kwa kuwa hatoshi kuendana na kasi serikali ya awamu ya sita.

**UVCCM PWANI**

"Sisi kama UVCCM mkoa wa Pwani, tulikuwa tunamheshimu sana Spika Ndugai, lakini kwa hili alilolifanya hapana, tunamwomba ajitafakari na ajiuzulu haraka nafasi yake ili kulinda maslahi ya chama chetu na serikali yetu ya awamu ya sita," alisema Samaha Seif, Mwenyekiti wa UVCCM mkoa wa Pwani.



**ASKOFU GWAJIMA**

Mbunge wa Kawe (CCM), Askofu Josephath Gwajima, alisema kauli aliyoitoa Ndugai haikuwa na nia njema na kama kiongozi anayeongoza muhimili muhimu anapaswa kujiuzulu.

"Spika anambebesha Rais Samia mzigo utafikiri yeye ndiye aliyekopa, hii sio sawa na ni kitu gani kilimfanya asikatae mkopo ulipofikishwa bungeni. Nia ya Spika haikuwa nzuri, inanipa picha kwamba anaweza kuwa na mtu wake au kuwa na kitu anachowaza. Pia kitendo kile cha mkuu wa mhimili kusema nchi itapigwa mnada ni cha kugombanisha Rais na wananchi ili wamchukie," alisema Askofu Gwajima.

"Spika alikuwa na nia ovu. Haijawahi kutokea mkuu wa mhimili katoka wazi kumpinga Rais wa nchi, kwa hiyo mimi nawaza ni mkuu wa mhimili gani ambaye anaweza kusema jambo A halafu akatoka kubadilisha. Namshauri Spika ajiuzulu na awaachie Watanzania wengine watakaomsapoti Rais ili twende kule tunakotakiwa twende."

"Hizi mambo za kusema nimekosa mimi nimekosa sana, ni kwamba ametambua kwamba amefanya kosa, basi ajiuzulu ili nchi iwe 'stable' na apatikane mtu mwingine anayeweza kumsaidia Rais."

Askofu Gwajima alisema Rais Samia Suluhu Hassan hatakiwi kubezwa na mtu yeyote kwa mkopo alioleta kwa ajili ya maendeleo kwenye nchi.

**LUSINDE**



Mbunge wa Jimbo la Mvumi jijini Dodoma, Livingstone Lusinde alisema utetezi alioutoa Spika Ndugai wa kwamba hotuba yake ilikatwa vipande si wa kweli na kwamba yeye alithibitisha kwamba kilichoripotiwa ndicho alichokisema.

"Ndugu zangu nimekuja mbele zenu kutoa tamko zito, baada ya kusikiliza hotuba yote ya Ndugai, aliyoitoa katika kikao cha Wanyausi, nimejiridhisha bila shaka kwamba hotuba ile ndiyo yenyewe aliitoa bwana Job, lakini hakuna kipande hata kimoja kilichokatwa, maana nimesikia katika utetezi wake anasema waandishi wa habari walikatakata, lakini mimi mwenyewe nimeipitia yote na nimejiridhisha pasi na shaka kwamba hakuna eneo hata moja limekatwa," alisema Lusinde.

"Lakini vile vile nikapitia hotuba ombi lake la msamaha kwa umakini mkubwa na hapa nataka niwaambie ndugu zangu wakazi wa Dodoma, bahati nzuri sisi Dodoma ndiyo wanufaika wakubwa wa serikali ya awamu ya sita. Rais Samia anamalizia Ikulu, lakini amehamia kabla hata haijaisha, kwa hiyo ni mwenzetu katika mkoa huu. Lakini kwa kujiridhisha kwamba Rais anatupenda wakazi wa Dodoma katika mgawo wa fedha alizokopa ambazo ndizo zinazosemwa, ametupatia mkoa wetu Sh. bilioni 17 ambazo zimejenga madarasa.

"Mimi nikiwa mbunge, mkazi na Mgogo ambao Spika alikuwa anaongea nao, Ndugai umefanya kosa, nakushauri leo (jana), hii jiuzulu isifike kesho uwe umejiuzulu nafasi ya Spika. Ukifanya hivyo utakuwa umetuletea heshima kubwa watu wa Dodoma na Watanzania wote."

**MRISHO GAMBO**

Mbunge wa Arusha Mjini (CCM) Mrisho Gambo, alisema: "Mheshimiwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, busara ikishindwa kufanya kazi, sisi wabunge tutasaidia kufanya maamuzi."



# Waziri aeleza umuhimu sekta binafsi mifugo

**Na Mbaraka Kambona**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema sekta ya binafsi ndiyo msingi wa maendeleo ya mifugo kwa sababu ushiriki wake umekuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza sekta hiyo nchini.

Waziri Ndaki alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea kiwanda cha kuchakata maziwa cha ASAS Dairies kilichoko mkoani Iringa.

Akiwa kiwandani hapo, alisema wawekezaji katika sekta ya mifugo kama ASAS wakiwa wengi, ni jambo zuri kwa maendeleo ya uchumi wa nchi kwa sababu uzalishaji wanaoufanya unachangia ukuaji wa pato la taifa na kujenga afya za wananchi.

"Serikali tunajivunia kuwa na wazalishaji wa maziwa kama ninyi. Serikali tunawaahidi tuko pamoja nanyi ili kuinua uchumi wa nchi yetu," alisema Ndaki.

Aliongeza kuwa serikali iko macho kuangalia changamoto zinazowakabili wawekezaji na kuhakikisha zinapungua makali yake ili kufanya kazi kwenye mazingira mazuri pamoja na wadau wao.

Kuhusu unywaji mdogo wa maziwa nchini, Waziri Ndaki alisema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, imeshaanza kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhamasisha unywaji wa maziwa ili wananchi wajenge utamaduni wa kunywa maziwa kwa wingi. Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha ASAS, Fuad Jaffer, aliipongeza serikali kwa kuweka tozo kwa bidhaa zinazotoka nje jambo ambalo limewapa wawekezaji wa ndani moyo wa kuendelea kuwekeza zaidi katika sekta ya mifugo.

Pia aliiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikisha vyuo vinavyozalisha maofisa ugani na taasisi za utafiti kuwa wabia na wachakataji wa maziwa ili kuzielewa changamoto ambazo wanazipata wafugaji.

Alisema kwa kufanya hivyo, wataalamu hao wanaweza kuwa msaada mkubwa katika kuelimisha wafugaji kuzalisha maziwa yenye ubora.




Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Ali Ngingite (katikati), akizungumza wakati wa kuchezesha droo ya kwanza ya kampeni ya MastaBata Kivyakovyako, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja Mwandamizi Kitengo cha Kadi, Manfred Kayala (kushoto) na (wapili kushoto) ni Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya kubahatisha Tanzania, Joram Mtafya. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## Mradi wa maji kunufaisha 3,600

**Na Frank Monyo**

ZAIDI ya wakazi 3,600 wa Kivule JICA Dar es Salaam, wapo mbioni kuondokana na shida ya maji baada ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kuufufua mradi wa maji eneo uliosimama tangu 2019.

Lengo la kufufua mradi huo ni kuboresha huduma ya majisafi kwa wakazi walio nje ya mtandao rasmi wa mamlaka hiyo.

Hili limethibitika kwa DAWASA kukamilisha kazi zilizolenga kuboresha mradi huo wa Kivule JICA, wenye uwezo wa kuhudumia zaidi ya wakazi 3,600 wa Kivule.

Akizungumza na Nipashe jana Jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Jamii wa DAWASA, Neli Msuya, alisema mradi huo uliosimama mwaka 2019, umefufuliwa baada ya kuona kuna uhitaji mkubwa kufuatia ongezeko la watu katika eneo hilo.

"Mradi huu umehusisha ufungaji wa pampu mpya na za kisasa za maji, uchimbaji na ulazaji wa bomba zenye ukubwa mbalimbali kwa umbali wa kilomita 4, lakini pia marekebisho katika mfumo wa umeme," alisema Msuya na kuongeza.

"Mbali na hayo ukubwa wa visima vinavyopatikana eneo hili vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita 12,000 na kingine lita 10,000 kwa saa ni sababu nyingine inayopelekea DAWASA kufufua mradi huu wa maji Kivule JICA. Kwa ujumla visima hivyo vina uwezo wa kuzalisha lita 290,000 za maji kwa siku," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Kerezange, Kata ya Kivule, Isdora Karanga, alisema wananchi wameupokea mradi huo utakaopunguza changamoto ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo.

"Tumepokea mradi huu uliofufuliwa na DAWASA kwa furaha kubwa, kwani tulikuwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa maji tangu mwaka 2019 mradi ulipoacha kufanya kazi huku wananchi wakitumia maji ya visima vya watu binafsi ambayo hayatoshelezi mahitaji yao na gharama zao ni kubwa," alisema Karanga.

# Kamati ya mawasiliano yatakiwa kutoa taarifa sahihi, kwa wakati

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Khatibu Kazungu, ameitaka kamati ya mawasiliano ya wizara kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa umma kwa kuwa ni haki ya wananchi kupata taarifa kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Agizo hilo lilitolewa jana kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Lusius Mwenda, wakati wa uzinduzi rasmi wa kamati hiyo iliyowakutanisha wajumbe kutoka kwenye idara na vitengo vya wizara wakati wa kikao kazi mjini hapa.

Alisema kamati ya mawasiliano ni kiungo muhimu cha mawasiliano kati ya idara au vitengo na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, ambacho ndicho kimepewa majukumu ya kuwasiliana na wadau muhimu wanaotarajia kupata taarifa kutoka kwenye kamati kwa ajili ya matumizi yao mbalimbali yakiwamo ya kiutafiti.

"Ni matumaini yangu kwamba kila mmoja wenu atawajibika kikamilifu kukusanya taarifa zinazohitajika kutoka kwenye idara husika kama mtakavyojadiliana na kufikia muafaka ili kuimarisha masuala ya mawasiliano kimkakati zaidi na wadau wetu wanufaike na uwapo wa kamati hii", alisema Dk. Kazungu.

Alisema miongoni mwa kazi za kamati hiyo ni kuratibu taarifa zinazohusu kitengo au idara, kukusanya na kuandaa taarifa zinazopaswa kutolewa kwa umma na kuziwasilisha kitengo cha mawasiliano serikalini, kuandaa taarifa za utekelezaji na kuandaa taarifa zitakazotumika katika majarida, vipeperushi na mabango.

Pamoja na majukumu iliyopewa kamati hiyo, alitoa angalizo la kufuata utaratibu wa kutoa taarifa kwa kuwa kuna watu maalumu waliopewa kibali cha kufanya kazi hiyo kwenye wizara, idara na taasisi za serikali. Kwa upande wa wizara, waliopewa jukumu hilo ni Katibu Mkuu na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini ambaye pia ni msemaji wa wizara.

Pia Dk. Kazungu alimpongeza, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Benny Mwaipaja, kwa kuandaa kikao kazi kinachoendana na mafunzo ya kuwajengea uwezo wana kamati ya mawasiliano kuhusu masuala ya mawasiliano ya kimkakati yatakayosaidia kufanikisha mawasiliano yenye tija kwa wadau wetu wa ndani na nje.

Kwa upande wake, Mwaipaja aliahidi kusimamia kamati vizuri na kutoa mrejesho kwa ngazi husika. Pia alisema wajibu wa kamati ni kuisogeza wizara karibu na wananchi na washirika wa maendeleo ili wajivunie uwepo wa wizara kwa kupata habari za kweli zitakazotolewa kwa wakati ili wazitumie kwa malengo yaliyokusudiwa.

Alisema kuwa katika kikao kazi hicho, wanakamati watapitia na kuchambua utekelezaji wa mkakati wa mawasiliano wa wizara ambao tayari umeridhiwa na kutiwa saini na Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji.

Mkakati huo, alisema umeainisha masuala ya msingi ya namna ya kuwasiliana na umma, aina ya ujumbe unaotarajiwa kutolewa, njia za kutumia kufikisha ujumbe husika, pamoja na tathmini na ufuatiliaji wa mawasiliano ili kuhakikisha kuwa ujumbe unawafikia wadau pamoja na kulinda taswira ya Wizara.

HABARI KITAIFA

# Wana-Tarime walilia Sirari kupandishwa hadhi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MADIWANI kutoka Tarafa ya Inchugu na wananchi wilayani Tarime, mkoani Mara, wameiomba serikali kusikia kilio chao cha muda mrefu cha kupandishwa hadhi mji wa Sirari.

Walisema kilio hicho ni cha tangu mwaka 2011 walipokitoa kwa aliyekuwa Waziri Mkuu kipindi hicho, Mizengo Pinda, alipofanya ziara wilayani Tarime na kufanya mkutano katika Kata ya Sirari na kutoa ahadi ya kupandisha hadhi miji ya Sirari na Shirati kuwa Mamlaka ya Miji.

Pia walitaka wananchi kujenga kwa kufuata utaratibu kutoka idara ya ardhi ili kuepuka kubomolewa nyumba zao ndani ya hifadhi za barabara na vichochoro.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki, katika kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, baadhi ya madiwani, John Mbusiro wa Kata ya Regicheri, Nashon Mchuma, Kata ya Gwitiryo, Amos Sagara, Sirari na Seronga Wangwe, Pemba, walisema kata ya Sirari pekee ina wakazi zaidi 50,000 ikiunganishwa na kata zinazozunguka mji wa Sirari za Gwitiryo, Regicheri na Pemba, kuna zaidi ya vijiji 15 na wakazi wanajenga kila kukicha.

Walisema Waziri Mkuu mstaafu Pinda alifika na kufanya mkutano uwanja wa tarafa Sirari na wananchi walitoa kilio cha kupatiwa mji wa Sirari kuwa mamlaka ya mji kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu huku mji ukiendelea kujengwa kwa kasi.

Walitaja mji huo kuwa na mahakama ya mwanzo, kituo cha polisi, OCD, kituo cha afya, kituo cha forodha, soko na viwanja zaidi ya 1,000 vilivyopimwa.

Walisema Sirari inastahili kupata hadhi ya mamlaka ili serikali iweze kuongeza kukusanya mapato kutoka katika miradi mbalimbali ya mji huo.

# Mwambe ataka fursa ya mikopo itumiwe

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MBUNGE wa Jimbo la Masasi ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Geofrey Mwambe, amewataka vijana, wanawake na watu wenye ulemavu wa jimbo hilo kuchangamkia fursa ya mikopo isiyo na riba ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara kukopa na kuanzisha miradi ya ujasiriamali ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Mwambe aliyasema hayo jana mjini hapa alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kata ya Sululu alipotembea kukagua mradi wa ujenzi wa soko la kisasa linalojengwa katika kata hiyo, ambalo msukumo wake umetokana na mbunge huyo baada ya kupokea kilio cha kutokuwapo kwa soko la kisasa na kutekeleza ahadi hiyo.

Alisema halmashauri imeshatangaza kutoa mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kupitia mapato yake ya ndani na katika fedha hizo, inatakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kukopesha makundi hayo ili waweze kuanzisha miradi ya kiuchumi itakayowawezesha kujikwamua kimaendeleo.

Alisema asilimia 10 ya fedha hizo, ni kwamba nne ni kwa ajili ya vijana, asilimia nne wanawake, na asilimia mbili inakwenda kwa vikundi vya watu wenye ulemavu na kupitia fedha hizo lazima vijana watumie fursa hiyo kwenda kukopa.

Mwambe alisema halmashauri imeshatangaza kukopesha Sh. milioni 100 kwa ajili ya vijana, wanawake pamoja na watu wenye ulemavu. Hata hivyo, chakushangaza tangu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo alipotoa tangazo hilo kupitia njia mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari hakuna hata kijana wa kiume au wa kike aliyejitokeza kukopa mkopo huo.

Alisema ni jambo la kushangaza kuona vijana wengi mjini Masasi wakikaa vijiweni bila kazi na hata pale inapotokea fursa kama hiyo ya mikopo isiyo na riba kwa ajili yao vijana hao bado ni wazito kujitokeza kukopa kuanzisha miradi ya ujasiriamali.

"Tunajenga masoko haya ndani ya Jimbo la Masasi, lengo letu kuona makundi haya yanainuka kiuchumi zaidi sasa inashangaza kweli halmashauri imetangaza kukopesha fedha Sh. milioni 100, lakini hadi sasa hakuna kijana hata mmoja aliyejitokeza kukopa hizi fedha...nendeni mkakope ni haki yenu vijana," alisema Mwambe.

Mwambe alisema amefanikisha ujenzi wa soko la kisasa la Kata ya Sululu pamoja na soko lingine linalojengwa Kata ya Mumbaka na kwa jumla yanagharimu shilingi milioni nane kila moja na hiyo itachochea ukuaji uchumi kwa vijana na wanawake na watu wenye ulemavu kupitia makundi yao ya ujasiriamali.

Awali Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Elias Ntiruhungwa, alisema katika mwaka wa fedha 2021/2022 halmashauri imetenga fedha hizo zipo kwenye akaunti Sh. milioni 100 kwa kuzitoa kwa vikundi vya wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

"Tumetangaza uwapo wa fedha zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kukopa, lakini ajabu ni kwamba hadi sasa miezi kadhaa imepita hakuna hata kijana au mwenye ulemavu aliyejitokeza kuja kukopa na fedha hizi ni zile asilimia 10 ambayo halmashauri inatakiwa kuzitoa kwa vijana, wanawake na wenye ulemavu," alisema Ntiruhungwa.

Alisema vijana wengi wilayani Masasi hawajui kutambua fursa zinazowazunguka ikiwamo mikopo kama hiyo ambayo haina riba na kwamba kama wangeitumia vyema fursa hiyo, wangeweza kujikwamua kiuchumi.



Mbunge wa Liwale, mkoani Lindi, Zuberi Kuchauka, akishiriki kubeba matofali kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Nayuru, mjini Liwale, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM Pwani yashukuru mikopo kuleta maendeleo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani, Ramadhani Maneno, amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akipata fursa ya kukopa aendelee kwa kuwa mikopo ndiyo inayofanya miradi ya maendeleo inayoonekana.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Halmashauri ya Kibaha Vijijini, vilivyojengwa kwa fedha za UVIKO-19.

Baada ya kukamilisha kukagua miradi hiyo ikiwamo ya shule za Sekondari Kawawa, Disunyara na Kilangalanga, Maneno alimshukuru Rais kwa kutoa fedha hizo ambazo zimetatua kero ya upungufu wa vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari.

"Fedha hizi za UVIKO-19 zimetusaidia sana kama kuna sehemu Rais Samia Suluhu anaweza kupata fedha akope aende kifua mbele tuko nyuma yake tutamuunga mkono," alisema Maneno.

Alisema fedha hizo pia zimejenga vyumba katika shule shikizi na kuondoa kero kwa wanafunzi waliokuwa wanatembea umbali mrefu kwenda shule na wengine kukatisha masomo kwa kushindwa kutembea muda mrefu.

Alitoa maelekezo kwa kila shule iliyonufaika kuyatunza na pia kuepuka kufanyia shughuli za sherehe kwenye madarasa hayo.

Mwenyekiti wa Halmashauri, Erasto Makala, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo ambazo zimepunguza uhaba wa madarasa.

Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Kibaha Vijijini, Fatuma Kisalazo, alisema kuwa wamepokea Sh. milioni 400 kwa ajili ya vyumba 20 shule za sekondari na Sh. milioni 200 madarasa 10.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Shukuru Lusanjala, alimweleza mwenyekiti huyo kuwa vyumba vyote 30 vilivyojengwa kwa fedha za UVIKO-19 vimekamilika tayari kwa kutumiwa na wanafunzi watakapofungua shule.

# Mbaroni kwa kukutwa na kipande cha jino la tembo

**Na Neema Hussein,**
KATAVI

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi linamshikilia, Jilangu Seni (33), mkazi wa Kijiji cha Misisi kwa tuhuma za kukutwa na kipande kimoja cha jino la tembo ambacho alikificha juu ya chumba chake.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Hamad, alisema tukio hilo lilitokea Januari 2, mwaka huu, katika kijiji cha Misisi, Wilaya ya Mlele, mkoa wa Katavi.

Kamanda Hamad alisema mtuhumiwa alikuwa amelihifadhi jino hilo kwenye mfuko wa salfeti na kulificha juu ya dari ya nyumba anayoishi.

Alisema thamani ya jino hilo bado haijatambulika na mtuhumiwa anaendelea kuhojiwa baada ya upelelezi kukamilika jalada lake litafikishwa ofisi ya taifa ya mashtaka mkoa wa Katavi kwa ajili ya taratibu zingine za kisheria.

Pia Kamanda Hamad aliwahimiza wote waliooshindwa kusalimisha silaha haramu kwa tarehe zilizopangwa, waendelee kuzisalimisha kwa kuwa hakuna atakaye salimika na msako unaendelea sasa katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema polisi wanaendelea kuwasaka popote walipo, kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wanaoendelea kumiliki silaha hizo.

Hata hivyo, Kamanda Hamad aliwapongeza wananchi wa mkoa huo kwa kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo kwa matukio mbalimbali ya kihalifu yanayotokea na kuendelea kuufanya mkoa kuwa salama zaidi.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Hamad akionyesha kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, kipande cha jino la tembo alilokamatwa nalo, Jilangu Seni (33) katika Kijiji cha Misisi, Wilaya ya Mlele. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

# Wananchi 74,599 wachanjwa Uviko-19

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI mkoani Shinyanga 74,599 wamepata chanjo ya UVIKO-19, kwa ajili ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Mratibu wa chanjo ya UVIKO-19 mkoani Shinyanga, Timoth Sosoma, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema kwa takwimu walizonazo hadi sasa, jumla ya wananchi 74,599 mkoani humo wameshapata chanjo hiyo na matarajio hadi kufikia Juni mwaka huu, wawe wameshachanja watu 1,196,153 sawa na asilimia 60.

"Mkoa wa Shinyanga tulipata chanjo zote za Johnson, Sinopharm, na Pfizer dozi 112,391, na wananchi waliopata chanjo ya Johnson ni 63,879, ya Sinopharm na Pfizer ni 10,720, na kufanya jumla ya wananchi waliochanjwa kuwa 74,599 mpaka sasa," alisema Sosoma.

"Changamoto ambayo inatukabili kwenye utoaji wa hizi chanjo, ni imani potofu ambayo imependikizwa ndani ya jamii kuwa zina haribu kizazi, pamoja na baadhi ya viongozi wa dini kuzipinga na kushawishi wananchi wasipate chanjo," aliongeza.

Alitoa wito kwa wananchi waliopata dozi ya kwanza, warudi kupata ya pili ili kujiimarisha zaidi kwa sababu wakifanya hivyo siku wakipata maambukizi ya virusi vya corona dozi hiyo moja haiwezi kuwasaidia.

Katika hatua nyingine alisema, kutokana na wananchi kuendelea kusuasua kupata chanjo hiyo kutokana na imani potofu, serikali kwa kushirikiana na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, wanaendelea kutoa elimu ya faida ya kupata chanjo hiyo, hasa katika maeneo ya vijijini ambako ndipo kuna changamoto kubwa.

Pia, alitoa wito kwa wananchi kupuuza maneno ya upotoshaji kuhusu chanjo hiyo na kujitokeza kwa wingi kwenye huduma za afya kuchanjwa ili siku wakipata maambukizi wasipate madhara makubwa tofauti na wale ambao hawakupata chanjo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga, Dk. Luzila John, alisema muitiko wa wananchi wanaofika kupata chanjo ya UVIKO-19 hospitalini hapo ni mzuri, kwa siku wanachanja watu 15 hadi 20.

Alisema kwa sasa katika hospitali hiyo ya rufani mkoani Shinyanga, hakuna hata mgonjwa mmoja ambaye amelazwa kwa tatizo la virusi vya corona, huku akitoa wito kwa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ya kujikinga na virusi hivyo.

# RC Gaguti aridhishwa Mtwara kufunguka

**Na Abdallah Khamis,**
MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amesema dhamira ya serikali ya kufanya mapinduzi katika sekta ya usafiri na usafirishaji, imeinufaisha mkoa huo kwa kuongezwa bajeti ya ujenzi wa barabara kutoka Sh. bilioni 8.5 kwa mwaka 2021 hadi Sh. bilioni 12.7 bajeti ya 2021/22. Alisema ongezeko hilo ni sawa na asilimia 172 na kuifanya Mtwara iwe rahisi kufikika kwa njia ya maji, barabara na anga tofauti na mikoa mingine.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Mtwara kwa mwaka wa fedha 2021/22.

"Tumeona Rais katika vipaumbele vyake ni kuifungua Tanzania na moja ya njia ya kuifungua ni pamoja na kuwa na miundombinu ya usafiri inayoweza kufikika kiurahisi na sisi Mtwara ni miongoni mwa mikoa hiyo tunayofikika bila matatizo," alisema Gaguti.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mtwara, Mhandisi Dotto John, alisema hadi Novemba 30, mwaka jana utekelezaji wa kazi za matengenezo kwa ujumla kwa barabara kuu na za mkoa huo, kwa mwaka wa fedha 2021/22, ulikuwa asilimia 32 ya malengo dhidi ya matumizi ya fedha yaliyofikia asilimia 10.00.

"TANROADS Mkoa wa Mtwara tunasimamia mtandao wa barabara wenye kilomita 1313.00, kilometa 284 kati ya hizo ni barabara kuu na 1029.00 ni barabara za mkoa, barabara kuu zote ni lami, pia kati ya kilomita 1029.00 za mkoa 144 ni za lami na 885.00 ni za udongo na changarawe," alisema.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22, Wakala wa Barabara ulitengewa Sh. 16,955,906,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa na Sh. 2,918,070,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya barabara za mikoa.


Akizungumzia miradi mikubwa ya kitaifa inayoendelea mkoani humo, alisema kwa sasa kuna ujenzi wa barabara ya Mtwara, Newala-Masasi wenye urefu wa kilomita 210, ikiwamo daraja la Mwiti.

Alisema mpango wa serikali ni kujenga barabara hiyo kwa awamu, ya kwanza ya ujenzi wa kiwango cha lami Mtwara-Minivata (kilomita 50) umekamilika kwa gharama ya Sh. 89,591,008,355.00.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22, serikali imetenga Sh. 3,000,000,000.00 kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa sehemu iliyobaki ambayo ni Mnivata - Newala Masasi (160km) na Novemba 25, 2021 serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imesaini mkopo wa Sh. bilioni 268.18 ununuzi.

Mbunge wa Mtwara Mjini, Hassan Mtenga, alisema wakati muafaka kwa serikali ya mkoa kuangalia uwezekano wa kujenga daraja la kisasa litakayounganisha mkoa wa Mtwara na Msumbiji kupitia mpaka wa Kilambo. Mbunge wa Nanyamba, Abdallah Chikota, aliitaka TANROADS kuacha urasimu na kuchelewa kuchukua uamuzi pale barabara za TARURA zinapotakiwa kupandishwa hadhi na kuwa chini yao.

Alisema barabara za TANROADS zinapotaka kushushwa hadhi suala hilo hufanyika haraka haraka lakini zinapotaka kupandishwa kwa ajili ya kuhudumiwa na mamlaka hiyo, kunakuwa na muda mwingi wa watendaji kujishauri namna ya kukubali.




Ukurasa 13

Salamu za Mwaka Mpya zilizochelewa!




**ADEM BAGAMOYO & UCHUMI WA KATI**
**Taasisi inayojibebesha jukumu kama la mkongwe Mzumbe katika sekta Elimu**

Ukurasa 12

BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
IJUMAA JANUARI 7, 2022
Nipashe

# Wanufaika TASAF Temeke walivyofikia maisha ‘poa’ kutoka enzi za umasikini

## • Malipo yanaingia ujasiriamali nao si haba

**Na Christina Mwakangale**

KINAMAMA wa Umoja wa Mshikamano kutoka Temeke mkoani Dar es Salaam ni kikundi ambacho baada ya kupita milima na mabonde, sasa wako katika tabasamu la kipato chao kuinuka.

Hapo kunatajwa kuwapo Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wanaoeleza namna walivyoinua kipato chao na familia na kuboresha maisha.

Wana kikundi hicho cha ujasiriamali wakizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam hivi karibuni, wanasema umoja huo umewainua na kuwaengua kutoka kikundi kinachoitwa ‘kaya maskini.’




Kikundi cha kinamama Mshikamano kutoka Temeke, mkoani Dar es Salaam, wakionyesha bidhaa zao kwenye Wiki ya Huduma za Fedha, iliyofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa mwaka jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Mariamu Mwisa, ni mwanakikundi anayesema walianza kwa mtaji mdogo baada ya kuwezeshwa na TASAF, kisha anaendelea: “Tulianza kuwezeshwa kama kaya maskini, tangu mwaka 2015...”

“Binafsi mimi sikusoma sana, kwamba nije kuwa mtu fulani. Ninapania kusomesha watoto wangu, ni ndoto ya kikundi chetu kwa ujumla kwamba iwapo sisi hatukusoma, usipowasomesha watoto wako, itakuwa nao wanatoka katika kaya maskini,” anaeleza Mariamu.

Anafafanua, kutokana na juhudi zao za sasa, wana matarajio makubwa watoto wao kujitosheleza kwa milo mitatu, pia wakisoma shule hadi ngazi ya chuo kikuu.

“Mshikamano wa kikundi tupo 10. Ukiwa katika kaya maskini, huwezi kuisaidia familia yako. Siku hizi hata wanao oana ni wanaoendana kimapato, kama ni wanaofanya kazi au waliosoma wote ni hivyo.

“Mfuko wa Maendeleo ya Jamii unatuwezesha, tunapokea kwa mwaka mara sita Sh. 36,000 kila baada ya miezi miwili. Huwezi ukadanganya kuhusu mpango huu, wengine wanalalamika kama hufuatilii na hupangilii pesa yako utaona ndogo.

“Mpangilio ni huu, hitaji la mtoto wa shule ya msingi mzazi unapewa sh 8,000, wa sekondari sh. 12,000 na kama una mtoto mchanga Sh. 4,000, hii pesa ni ya kila mwezi. Wanachojali TASAF ni idadi ya watoto ulio nao na wanaosoma shule. Tunaishukuru TASAF kwa mpango huu umetuwezesha tukafika hapa,” anaongeza Mariamu.

Anasema kikundi hicho kinachofanya shughuli zake wilayani Temeke kilianza kwa mpango wa kuweka kipato kila mwezi kwa mfumo wa hisa, umewainua sana.

“Mwanzoni tulipoanza tulikuwa tunajitahidi kununua hisa ya 2,000, ambayo saa nyingine hata kama huna unajitahidi ili uongeze mtaji. Tukajichanga na mratibu wetu akakubali kumuita mkufunzi wa kazi za mikono kutufundisha kutengeneza viatu vya kimasai, shanga, vikapu, pilipili, chachandu na siagi.

“Tulipo na ofisi ndipo tunauzia biashara zetu, ila kuna siku tunaamua tuzunguke minadani na maofisini kuuza bidhaa zetu. Huwa tunanunua shanga nyingi katika maonyesho...soko ni changamoto.” Anafafanua na kuendelea:

“Uamue upitishe mtaani, lakini ukiuza biashara kama hii eneo unalofahamika, ujiandae kukopwa. Tungekuwa kama Mwenge (Dar es Salaam) wale wauza vinyago wana eneo maalumu, wamachinga wanatengewa eneo lao na sisi wenye vitu vya asili kaya maskini tupatiwe eneo.”

Inaelezwa hadi sasa kuna zaidi ya kaya 240 masikini zinazohudumiwa na TASAF mkoani Dar es Salaam, ambazo zimeshajengewa uwezo kuanzisha miradi midogo inayowasaidia kuboresha hali zao kimaisha.

“Tunashukuru sana TASAF. Imetutoa mbali, tulikuwa kaya maskini, lakini sasa tunaimarika na kupitia wao ambao kila mwezi tunapewa pesa na kutunza Sh. 5000 na tumeanzisha kikundi cha watu 15 kila mmoja ana mradi wake na leo tumesajiliwa,” anaeleza Mariamu.

Mnufaika wa TASAF, Tausi Khalfani, ambaye pia ni Katibu wa Kikundi, anaiambia Nipashe kwamba awali kaya yake ilikuwa maskini kiasi cha kushindwa kusomesha watoto na kuwadumia kimaisha, lakini sasa imebaki historia.

Kaimu Mratibu wa TASAF wilayani Ilala, Lilian Shoo, anachangia kuwa, miradi hiyo imebadilisha hali kimaisha ya wanifaika, ambao wameanzisha miradi ya kutengeneza vikapu na bidhaa nyingine za kuboresha familia na uchumi wao.

UCHUMI

ADEM BAGAMOYO & UCHUMI WA KATI

# Taasisi inayojibebesha jukumu kama la mkongwe Mzumbe katika sekta Elimu

- CEO Dk. Masanja: Tupo tunachangia Tanzania ya Viwanda
- Wajigamba kuondoa pengo la zama walipopelekwa Uingereza



JUKUMU LA KITAALUMA LIKIENDELEA ADEM. **PICHA: MTANDAO**

**Na Julieth Mkireri, aliyekuwa BAGAMOYO**

KUNA mengi yanayoshughulikiwa kuboresha uchumi kitaifa na kimataifa. Eneo mojawapo ni mfumo wa uendeshaji nchi na usimamizi wake, katika tafsiri ya utawala, uongozi na menejimenti, ambayo ndio ufunguo unaosimamia kila kilichoko cha kila siku.

Msingi wa dhana menejimenti, unaangukia katika namna mtu (au watu) anaandaa, anaratibu pia kusimamia jambo, ndani yake nyenzo kuu ikiwa namna anavyochukua uamuzi na hatua kwa haraka zenye busara, iwe katika taasisi au eneo fulani la kiutendaji.

Hapo ndipo kunashuhudiwa umuhimu wake katika kuandaa uchumi wa nchi, kwani ikirejewa historia ya nchi, umuhimu unaonekana miaka minne tu baada ya kupatikana uhuru, serikali ilipoanzisha chuo mahsusi cha menejimenti na utawala - Mzumbe, mwaka 1965 na hata miaka ya baadaye, kikaanzishwa kingine cha mafunzo na uongozi wa chama, TANU na baadaye CCM, Kivukoni jijini Dar es Salaam, ambayo leo hii ndio Taasisi ya Mwalimu Nyerere Kivukoni, Dar es Salaam.

Falsafa ya Muasisi wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, ilikuwa utoaji elimu inayolingana na uhitaji wa jamii ya Watanzania, akiibatiza kwa jina Elimu ya Kujitegemea.

**MZIZI WA MANTEP**

Hapo hasa ndio mzizi wa serikali kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Uongozi kwa Viongozi wa Elimu (MANTEP), ambayo baadaye mwaka 2001, ilibadilishwa jina na muundo kisheria kuwa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu.

Ni muundo unaolenga uanzishwaji Mafunzo ya Uongozi na Menejimenti ya Elimu kwa Viongozi na Wasimamizi wa Elimu nchini.

Kabla ya mwaka 1978, viongozi na wasimamizi wa elimu nchini walikuwa wanapelekwa Uingereza katika Chuo cha Moray House, ili kunolewa kwa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa elimu.

**CEO ADEM**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dk. Siston Masanja, anasema gharama ya kuwasomesha watumishi nje ya nchi ilikuwa kubwa zaidi ikiigharimu serikali fedha nyingi na inawaangukia watumishi wachache.

Anasema mbadala wake, serikali ilianzisha Mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu nchini na ndio mwanzo wa kuanzishwa taasisi ya MANTEP, iliyoko Bagamoyo, ambayo ilibadilishwa kuwa ADEM mwaka 2001. Imeshafungua matawi Mwanza mwaka 2010 na Mbeya (mwaka 2015).

Wakala huo una majukumu ya kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uongozi na usimamizi wa elimu, ili kuzishauri wizara zinazohusika na elimu kuhusu uongozi na usimamizi wa taasisi za elimu nchini.

Pia, inatoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi na usimamizi wa elimu kwa viongozi na watendaji wa sekta husika nchini.

**WALENGWA NA MAFUNZO**

Walengwa wa Mafunzo ya ADEM ni pamoja na walimu wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, viongozi na wasimamizi wa elimu katika ngazi ya shule, kata, halmashauri, mkoa na taifa.

Dk. Masanja anasema, hadi sasa viongozi wanaosimamia sekta ya elimu nchini, takribani asilimia 90 ya viongozi na Wasimamizi wa Elimu wamepata mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na muda mfupi yanayotolewa ADEM.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ADEM, Dk. Siston Masanja, anaeleza takribani miaka 43 imepita, wakala unatoa mafunzo ya muda mfupi.

Pia, kuanzia mwaka 1990, ADEM ilianzisha mafunzo ya muda mrefu ambayo ni Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu (Diploma in Education Management and Administration).

Aidha, anasema mwaka 2014 yaliongezwa mafunzo ya Stashahada ya Udhibiti Ubora wa Shule (DSQA) na Astashahada ya Uongozi, Usimamizi na Utawala wa Elimu (CELMA).

Kwa mujibu wa Dk. Masanja, mafunzo ya stashahada hutolewa kwa miaka miwili na mafunzo ya astashahada ni ya mwaka mmoja.

"Kumekuwapo ongezeko la walimu wanaojiunga na mafunzo ya muda mrefu ya kozi za uongozi na usimamizi wa elimu kutoka walimu 30 katika miaka ya 1990 chuo kilipoanzishwa hadi 1,985 mwaka 2021. Mafunzo haya yanawasaidia kuwa viongozi na wasimamizi bora wa elimu" anaeleza.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo, anaongeza kwamba kuna walimu 1,419 wamejiunga na ADEM na kuhitimu mafunzo ya Stashahada ya Ukaguzi wa Shule, ambayo sasa inafahamika Stashahada ya Udhibiti Ubora wa Shule kuanzia Mwaka 2014, kozi hiyo ilipoanzishwa.

Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2021, anasema ADEM imeendesha mafunzo ya muda mfupi yenye lengo la kuimarisha usimamizi wa ufundishaji na kujifunza katika ngazi ya shule na vyuo, Dk. Masanja akisema inanuia kuendana na mahitaji ya kuufikia uchumi wa viwanda, unaochagiza maendeleo ya nchi katika uchumi wa kati.

Wanufaika wa mafunzo hayo ya muda mfupi, wanajumuisha maofisa elimu taaluma wa wilaya 184, wathibiti ubora wa shule183 na moafisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) 20.

Dk. Masanja anafafanua kuwa, ADEM imeendesha mafunzo ya muda mfupi ya Udhibiti Ubora wa Ndani na Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa maofisa elimu wa mkoa, maofisa elimu taaluma ngazi ya mkoa na maofisa elimu msingi wa halmashauri 647.

"Mafunzo haya ya Uthibiti Ubora wa Shule wa Ndani yametolewa pia kwa walimu wakuu 9,302 kutoka halmashauri zote za Tanzania Bara," anaeleza.

**MAFUNZO YA KIUCHUMI**

Mafunzo mengine ya muda mfupi yaliyoendeshwa na ADEM kati ya mwaka 2020-2021 pekee, yanajumuisha uongozi, uandaaji na usimamizi wa mpango wa jumla wa maendeleo ya shule na ufuatiliaji wa rasilimali kwa wajumbe wa kamati za shule 12.

Mtendaji Mkuu wa ADEM, anaeleza mafunzo mengine ni ya uandaaji mpango mkakati na usimamizi wa fedha na matumizi kwa wajumbe 315 wa timu za menejimenti za vyuo vya ualimu vya serikali nchini.

Aidha, anataja suala la utoaji mafunzo ya uongozi na usimamizi wa ufundishaji na kujifunza, kwa wajumbe 245 wa timu za menejimenti za vyuo vya ualimu vya serikali nchini,

**MAENEO MENGINE**

Dk. Masanja anataja mafunzo mengine ya muda mfupi yaliyotolewa na ADEM katika kipindi cha mwaka 2015 na 2019, ni uimarishaji stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa walimu 35,233 wa darasa la kwanza hadi la nne, kwa wanaofundisha lugha na hisabati.

"Mafunzo hayo yalihusu pia walimu wanaofundisha wanafunzi wa elimu ya msingi nje ya mfumo rasmi (MEMKWA) kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara, na mengine kwa walimu Wakuu na Maofisa Elimu Kata 13,850, na mafunzo kuhusu miongozo yao ya shule kwa wakuu wa shule 1,200", anafafanua.

**SAFARI YAO INAKOELEKEA**

Dk. Masanja anaeleza katika kuhakikisha ADEM inaendelea kufanya vizuri zaidi katika utoaji mafunzo yake, imejipanga kuongeza idadi ya udahili kutoka 1,985 waliopo sasa hadi kufikia 3,050 mwaka 2026.

Anasema lengo ni kuimarisha usimamizi wa utoaji elimu bora katika ngazi zote za elimu inayokua kwa kiwango kikubwa, akisisitiza inaendelea kusimamia misingi ya utoaji elimu bora kwa kutoa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa walimu kuwa viongozi na wasimamizi wa elimu nchini.

"Matarajio ADEM itaendelea kuwa kitovu cha mafunzo ya Uongozi yenye kuleta tija kufikia Dira ya Taifa ya kujenga Uchumi wa Kati unaoambatana na maendeleo ya viwanda kufikia mwaka 2025," anasema Dkt Masanja.


Kwa mujibu wa Dk. Masanja, wanalenga kuanzisha mafunzo mapya yanayoendana na mahitaji ya jamii na sekta ya elimu nchini kwa kuzindua mtaala wa Shahada ya Usimamizi wa Udhibiti Ubora wa Elimu na Uongozi, mafunzo ambayo hivi sasa hayapo nchini.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akihutubia kwenye moja ya mahafali ya Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), Bagamoyo. **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Salamu za Mwaka Mpya zilizochelewa!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

INGAWA ni siku ya saba tangu kuuanza mwaka huu mpya wa 2022, lakini bado nawiwa kukutakieni wasomaji wangu heri ya Mwaka Mpya, ingawa Jumamosi iliyopita nasikia mlifanya yenu mpaka wengine wakasahau kuwa mwaka umeanza.

Ni safari nyingine ya sekunde 31,536,000 ya kujipima kama tutatoboa mpaka 2023 au la, kwa sababu wanasema kumaliza mwaka siku hizi ni tabu, kwamba kifo cha sasa ni kama maji, yatokako yaendako hakujulikani...!

Tukitazama nyuma tulikotoka, kila mtu anajua alijikwaa wapi alikanyaga mbigiri wapi, na kama alianguka na kuinuka sawa na kama alianguka na kukaa hapo hapo yote heri, lakini tunajua tulikotoka na sasa tutazame tunakokwenda.

Mwaka jana ulikuwa ambao nchi hii ilipitia mabadiliko, ambayo yanaacha historia, kuwa iliondokewa na Rais akiwa madarakani na ikapata Rais mwanamke kwa mara ya kwanza katika historia.

Nani alitarajia kuwa tungekuja kuongozwa na Rais mwanamke? Nasikia tu kuwa mtabiri mashuhuri, marehemu Shekhe Yahya Hussein, alipata kutabiri haya kuwa atatokea Rais ambaye hatamaliza mihula miwili na kufuatiwa na mwanamke.

Kudra za Mwenyezi Mungu ndizo zilisababisha sasa tuna Rais anaitwa Samia Suluhu Hassan. Na pengine mazoea kuwa haiwezekani nchi hii ikaja kuongozwa na mwanamke, ndiyo yanayofanya tunashuhudia haya yanayoendelea hivi sasa.

Tumeshuhudia na tunashuhudia, watu wanaoamini katika mfumo dume wakiibuka na kutoa matamko ambayo hatukuyazoea sisi ya kama kutaka kumtingisha Chifu Hangaya, wakijisahau kana kwamba Katiba inampa kila haki ya kuwa hapo alipo, licha ya jinsia yake.

Wanajisahaulisha kuwa, wapo watu wanaomuunga mkono na ambao ni wengi kuliko wao hao wachokonozi, wanaotingisha kibiriti kutaka kujua kama kimejaa njiti au la, lakini haki ya Mungu wanapoteza muda wao.

Walizoea kukaripiwa na kusemwa na hata kutumbuliwa hadharani huku wakitazamwa na familia zao, lakini Chifu keshasema yeye si wa hivyo, ataendelea kushikilia kalamu yake akichora nukta mkato na nukta.

Mwaka uliokwisha, tulishuhudia wale kambale wadogo wakiibuliwa kwenye tope na kuwekwa mahali stahiki.

Mimi na wenzangu tunaamini kwamba, mwaka huu utakuwa mwaka mzuri wa watu kujipanga kuleta maendeleo kwa utulivu. Tunaamini mabadiliko ya kisiasa yatafanyika, ili kuweka mambo tambarare na ifikapo mwaka 2025 kila atakayesimama kwa miguu yake, basi aanguke tu akitaka na si vinginevyo.

Sisi pia tunaamini na tunataka Chifu Hangaya aachwe afanye yake, kwa kuwa Katiba na kudra za Mwenyezi Mungu zimetaka awe kiongozi wetu, hivyo hatutakubali mtu amtingishe, eti kwa sababu ana uchu wa madaraka, ila yeyote anayetaka kukalia kiti cha Chifu asubiri 2025.

Na ajue kufika huko kusiwe kwa kukanyaga. Chifu Hangaya mwaka huu akaitazame tena safu yake, nani wa kafunga mkanda kwenye kiti chake katika safari hii na hayupo tayari, ili amuache nje.

Wananchi Watanzania wenzangu, katika ujumbe wangu huu wa Mwaka Mpya, napenda kuendelea kukutakeni mliangalie kwa macho manne hili tatizo la UVIKO-19, nadhani mnadhani limemalizika na ndiyo sababu hamtaki kuchanja.

Hivi sasa hiki kirusi cha Omicron ni hatari sana na kinasambaa kama moto wa nyika, kudharau kwako kuchanja ni kudharau maisha yako na kitakutafuna tu na acha kikutafune ukiendelea kusikiliza wahafidhina wasiotaka kuchanja.

Najua tatizo kubwa ni imani ya watu katika chanjo na hasa kutokana na kwamba walio kuwa wanapinga chanjo mwaka juzi ndio hao hao wanapewa jukumu la kuhubiri kuwa chanjo ni salama na inafaa, watu wanachanganyikiwa na ndiyo sababu wanakimbia vituo vya chanjo. Tufanyeje? Alamsiki!

BIASHARA

# Binti shule ya msingi tayari ana kipaji cha ujasiriamali wa ufundi cherehani

- Kaingia na ujuzi tangu darasa la kwanza
- Hajui kutumia tepu, kukadiria hakosei
- Ametumia cherehani bila ya kufunzwa
- Pesa ya matumizi ni mtaji wa vitambaa



Mtoto mbunifu Pascalina Mpanji (14), akiwa na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Serengeti, Bupe Thomas (kulia) na mlezi wake, Melisiana John.



Pascalina Mpanji, akiwa na kazi yake ya ushonaji. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA.**

**NA KULWA MZEE**

MIKAKATI ya Serikali ni kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu ya kujitegemea wakiwa shuleni, ili kuwawezesha kujitegemea kwa kuwa na ujuzi mara baada ya kumaliza elimu ya msingi, sekondari ama chuo.

Kukosekana kwa elimu ya kujitegemea kuanzia shule ya msingi, kunawafanya vijana wengi wanaposhindwa kuendelea na masomo, wanakuwa hawana kazi nyingine ya kufanya mwishowe wanajiingiza katika makundi mitaani.

Ni dhana ambayo aliibuni Rais Julius Nyerere Mwaka 1967, akiipa jina la Elimu ya Kujitegemea, ikiwa na ufafanuzi kwamba kila ngazi ya elimu iwe inajitegemea, mathalan mhitimu wa elimu ya msingi asijitambue kafeli, bali ameishia darasa hilo na liwe limemsaidia.

Pia, elimu isizae watumishi wa ofisini tu, vivyo hivyo maudhui ya elimu, yafanane na uhalisia wa maisha ya umma na msomi wa elimu ya nchi daima arejee kutumikia jamii yake, pia naye ajitegemee.

Hakuna ubishi kwamba sasa kuna watoto wengi wana vipaji mbalimbali, lakini kwa kutotambua vipaji vyao, ama kwa kukosa mbinu za kuwainua na kukuza vipaji hivyo, wanaachwa hivyo hivyo vipaji vinakufa.

**'DOGO' MJASIRIAMALI**

Katika Shule ya Msingi Serengeti iliyopo Kivule wilayani Ilala, Dar es Salaam kuna mwanafunzi anayeingia wa darasa la sita, Pascalina Mpanji (14), ambaye hadi sasa ni mtaalamu wa kushona nguo za kike na za kiume kwa kutumia sindano ya mkono na kukata kitambaa kwa kutumia wembe na anaweza kuvuna kipato kutokana na ufundi wake.

Pascalina anaiambia Nipashe kwamba, alipokuwa umri wa miaka saba pekee, alianza kukata vitambaa na kushona nguo ndogo za watoto, kwa kutumia sindano ya mkono na alikuwa akifanya hivyo kila anapokuwa kamaliza kufanya kazi za nyumbani.

Mwanafunzi huyo alitokea Mkoani Songwe kwa wazazi wake akiwa hajaanza shule na kuja Dar es Salaam mwaka 2016 kwa dada yake aliyemtaja kwa jina Melesiana John, aliyemuandikisha shule na kuanza darasa la kwanza mwaka 2017.

"Hakuna anayeshona nguo nyumbani kwetu, nilianza kwa kujaribu nikiwa na miaka nane, nilikuwa naokota vitambaa kwa mafundi, narudi nyumbani nashona nguo, mishono naibuni mwenyewe.

"Dada alivyoona nashona akawa ananipa vitambaa na wakati mwingine ananipa fedha naenda kununua kwa mafundi vitambaa vilivyobakia kwa wateja wao," anasimulia Pascalina.

Anasema kila alipopewa fedha kwa ajili ya matumizi ya shule, hakuitumia, badala yake anaenda kununua vitambaa na uzi kwa ajili ya kushona nguo na ameshawahi kushona nguo nyingi akawagawia ndugu zake wanavaa.

Pascalina anasema, mishono anaifahamu baadhi anataja kuwa: soro ya kuvuta rinda, soro ya kumwaga na mshono aliouita 'nguva' na anatumia siku moja kukata na kushona gauni moja, kutokana na muda wake kuwa mfupi kubanana na ratiba ya shule.

Anasema anapotoka shule, anaosha vyombo nyumbani na baada ya kumaliza vyombo, usiku unapoingia ndiyo anaanza kushona nguo alizo nazo.

Mtoto huyo anataja nguo anazojua kuzishona ni magauni, suruali, kaptura, lakini hajui kutumia tepu kumpima mvaaji, hivyo anachofanya ni kumuangalia mvaaji anamkadiria vipimo kwa kichwa, kisha anashona nguo na inamtosha.

Binti huyo, anasema hajazoea kushona shati, japo alishawahi kushona na akizoea atashona vizuri kama anavyoshona gauni.

"Nikimaliza elimu yangu ya msingi, napenda kuendeleza kipaji changu na ikiwezekana kama nitachaguliwa kwenda Chuo cha Ufundi nitafurahi zaidi nikaendelee kujifunza.

"Kuna siku nilikuta cherehani kwa dada mmoja namfahamu, yule dada alipoinuka niliokota kitambaa pale chini nikakaa katika mashine nikashona, nikaona kumbe naweza kutumia hata cherehani bila kufundishwa," anasema Pascalina.

Anasema, katika kushona anakabiliwa na changamoto ya vifaa ikiwemo vitambaa, mkasi, tepu ya kupimia, cherehani, meza na eneo la kufanyia kazi, akipata msaada wa vitu hivyo kazi zake zitakuwa bora zaidi.

**MWALIMU MKUU**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Serengeti, Bupe Thomas, anaiambia Nipashe kuwa mwanafunzi wake uwezo wake darasani ni wa wastani na hayuko vibaya.

Anasema, alibaini kipaji cha mwanafunzi huyo mwaka 2019 akiwa darasa la tatu, alipokuwa akipewa kazi katika somo la stadi za kazi, kesho akikabidhi anakuwa ameshona nguo ya mtoto.

"Walimu tulivyomfuatilia kwa karibu tukaanza kumnunulia vitambaa tunampa anashona, yalipotokea mashindano ya watoto wenye vipaji kwa shule 11 za kata ya Kivule, tulikuwa tukimpeleka na anaibuka mshindi.

"Wapo wanafunzi wengine wana vipaji vya kuimba, kukimbia na wachoraji, lakini kipaji cha Pascalina ni cha pekee. Tunatafuta wafadhili wa kuweza kumsaidia kukuza kipaji chake, anafanya kazi zake kwa muda mfupi na kazi nzuri," anasema Mwalimu Mkuu.

Mwalimu anasema yuko tayari kumnunulia vitambaa vizuri, mikasi, tepu ili aanze kukata nguo kwa vipimo kuboresha kazi zake.

"Mpaka sasa hivi tumeshamnunulia mkasi na vitambaa kiasi anavyotumia kushona nguo lakini naahidi kuendelea kumsaidi kwa vitu hivyo ambavyo nimesema," anasema mwalimu Bupe.

**MLEZI WAKE**

Dada yake Melisiana John, anasema alianza kukaa na binti huyo mwaka 2016, alipomtoa Songwe akiwa na miaka nane hajaanza elimu ya msingi, lakini alipokaa naye akamuona mbunifu akamwandikisha darasa la kwanza, mwaka 2017 akaanza masomo.

Anasema, alianza darasa la kwanza akiwa na miaka tisa, alikuwa anajua kushona na muda wake mwingi hutumia kushona na kumsaidia kazi ndogo ndogo za nyumbani.

Melisiana anasema mdogo wake hana muda wa kucheza akiwa nyumbani zaidi ya kusoma kidogo na kufanya kazi zake za kushona.

"Nilipomuona kipaji chake nikaanza kumpa muda wa kutosha ili aweze kushona nguo, nampa fedha za kununua vitambaa na uzi, watoto wangu wawili anawashonea nguo.

"Naomba Serikali imwendeleze akuze kipaji chake kama inavyokuza vipaji wa wasanii nchini , uwezo wangu si mkubwa lakini akimaliza darasa la saba nitamnunulia cherehani," anasema dada yake.

Akizungumzia changamoto anazokutana nazo, anasema changamoto za kimaisha zipo lakini kwa uwezo wa Mungu wanazishinda.





## Tanzania, Burundi zajadili ushirika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MRAJISI wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dk. Benson Ndiege, jana alifanya kikao kwa njia ya mtandao na Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Dk. Jilly Maleko, kuhusu ushirikiano wa kiushirika kati ya nchi hizo mbili.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa alipofanya ziara nchini Burundi, Julai 16 na 17, mwaka jana.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Dk. Ndiege alisema katika ziara hiyo, Rais Samia alielekeza Tanzania na Burundi kubadilishana uzoefu katika sekta za kilimo na mifugo hususan kwenye uendeshaji wa vyama vya ushirika na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

"Ni matumaini yangu kupitia kikao hiki tutaweza kujadili vyema maeneo ya ushirikiano katika shughuli za vyama vyetu vya ushirika na vyama vilivyoko nchini Burundi," alisema.

Dk. Ndiege alisema tume ipo tayari kuhamasisha vyama vya ushirika kwenda kubadilishana uzoefu wa ushirika nchini Burundi na wao kuja kujifunza namna ushirika unavyofanya kazi nchini.

Alibainisha kuwa tume imekuwa ikifanya kazi ya kuviunganisha vyama hivyo na fursa mbalimbali zikiwapo za masoko na uwekezaji ndani na nje ya nchi.

Mrajis huyo alisema kuna vyama vya ushirika 9,185 nchini na kati ya hivyo 4,039 ni vyama vya ushirika wa mazao.

Balozi Maleko alisema changamoto ni ubalozi unapohamasisha Watanzania kulitumia soko la mchele nchini Burundi kutokana na wanunuzi kuwa kwenye ushirika.

"Hivyo changamoto hii inaweza kutatuliwa iwapo kutakuwa na ushirikiano wa kiushirika kati ya nchi hizo mbili.

"Mtanzania akiingiza mchele Burundi anakutana na uongozi wa chama cha ushirika na anaweza asiuze kwa faida kutokana na kukosa 'connection' nzuri kwa kuwa wenzetu wana ushirika kwenye mazao ya nafaka," alisema Balozi Maleko.

# Serikali yapokea vifaa kujikinga na corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekabidhi vifaa vya kujikinga na UVIKO-19 kwa mikoa 12 ya Tanzania Bara na mitano ya Zanzibar ambavyo vimetolewa na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC).

Vifaa hivyo vimetolewa kupitia Shirika la Kimataifa la Lishe (NI) ikiwa ni jitihada za kuwakinga watoa huduma ya afya wakati wa kampeni ya utoaji wa huduma ya matone ya vitamini A nchini.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo kwa wawakilishi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, alisema vifaa hivyo vitawasaidia watoa huduma za afya walio mstari wa mbele wakiwamo watoa huduma za afya ngazi ya jamii (CHW).

Dk. Sichalwe alisema kutokana na changamoto ya UVIKO-19, serikali inaendelea kuwapatia vifaa vya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo watoa huduma walioko katika vituo vya afya ili kuwawezesha kuendelea kutoa huduma za afya kwa ufanisi.

"Vifaa hivi vimeanza kutolewa katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Morogoro, Katavi, Mwanza, Kilimanjaro, Shinyanga, Simiyu, Singida, Tabora na Tanga na mikoa yote mitano ya Tanzania Visiwani.

"Mikoa hiyo imechaguliwa kwa sababu ilikuwa na ufanisi duni katika utoaji wa huduma za afya, hivyo kupitia msaada huu, itaimarisha kiwango cha ufanisi katika utoaji wa huduma za matone ya vitamini A kwa watoto wengi zaidi," alisema Dk. Sichalwe.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TFNC, Dk. Ray Masumo, aliishukuru serikali ya Canada kupitia shirika lake la Nutrition International kwa kuendelea kuiunga mkono serikali katika vita dhidi ya UVIKO-19 na changamoto nyingine za lishe.

Dk. Masumo alisema vifaa hivyo vitawasaidia watoa huduma ya afya waliopo mstari wa mbele katika kutoa huduma za afya ikiwamo huduma ya mwezi wa afya na lishe ya mtoto. Alisema malengo yaliyopo ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025, watoto wote nchini wafikiwe na huduma ya matone ya vitamini A kupitia vituo vya afya vilivyoko nchini.

Mkurugenzi Mkazi wa Nutrition International, Dk. Daniel Nyagawa, alisema wamechukua uamuzi wa kutoa vifaa kwa serikali ikiwa ni kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazochukuliwa katika kupambana na UVIKO-19.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Dk. Mwanahamisi Hassan, alisema vifaa hivyo vitawasaidia watoa huduma za afya waliopo mstari mbele katika vita ya UVIKO-19, hivyo akawaomba wadau wengine kujitokeza katika kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na serikali katika vita hiyo.

Katoni 6,000 za barakoa na vitakasa mikono lita 6,000 vyenye gharama ya Sh. milioni 57 vitasambazwa katika mikoa 17 ikiwamo 12 ya Tanzania Bara na mitano ya Zanzibar.




Wafanyakazi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wakibomoa majengo yaliyoko jirani na jengo la kitega uchumi la hoteli jijini humo jana, ambalo linatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni baada ya kukamilika ujenzi wake. Uongozi wa Jiji hilo ulilipa fidia kwa mmiliki wa jengo hilo ili kupisha nafasi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Watekeleza mradi udahili wa watoto wenye ualbino, wasioona

**Na Peter Mkwavila,** MPWAPWA

CHAMA cha Wasioona Tanzania (TLB), Chama cha Watu wenye Ualbino (TAS) na Jumuiya ya Wasioona Zanzibar kwa pamoja vimetekeleza mradi wa kudahili watoto 344 wasioona na wenye ulemavu wa ngozi na kuwapatia huduma za elimu na afya.

Pia vyama hivyo kwa pamoja vimetekeleza mradi huo kwa kuwafikia watoto hao majumbani ili kuwadahili na kuwawezesha kupata haki ya msingi ya elimu jumuishi na huduma za kiafya. Akizungumza na Nipashe katika kijiji cha Ghambi wilayani Mpwapwa, Mratibu wa Mradi wa Kufadhili Watoto wenye Ulemavu wa My Right (SRF) toka Sweden, Emmanuel Mhehwa, alisema watoto 344 ambao kati yao ni wenye ulemavu wa kutoona na ngozi wamewezeshwa na mradi huo.

Mhehwa alisema lengo kuu ni kuwawezesha misaada mbalimbali ikiwamo kuhakikisha wanapata haki zao za msingi za kusoma na afya sawa na wale wasio na ulemavu.

"Mradi ulianza mwaka 2018 hadi 2021 ikiwa ni awamu ya mwisho kwa mwaka wa 2021 umewafikia watoto 344 ambao ni wenye ulemavu wa kutoona na ngozi kwa kuwapatia huduma mbalimbali ikiwamo kuwaandikisha shule na huduma za kiafya," alisema.

Nao watoto wenye ulemavu wa kijiji cha Nh'ambi kitongoji cha Mvamiyo, walisema kuwa mradi huo umewawezesha kupata huduma mbalimbali wanazostahili ikiwamo elimu ambayo awali waliikosa.

Egra Magondo (16) na Grenc Shedrak (12) ambao ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Buigiri ya Wasioona iliyoko Wilaya ya Chamwino, walisema awali hawakuwa na uhakika wa huduma za msingi kama ilivyo kwa watoto wengine.

"Kwa kweli tunashukuru mradi wa My Right kwa kutuona na kutuwezesha kupata huduma mbalimbali hususani hii ya elimu na afya. Ni imani yetu tutaweza kusoma na kufikia hatua ya juu zaidi," walisema.

Baadhi ya wazazi wenye wa watoto wenye ulemavu walisema mradi huo umewawezesha kutua mzingo wa kuwasomesha na wanaamini kuwa familia zao zitapata ukombozi kupitia kwa watoto hao.

Mmoja wa wazazi hao, Neema Sigila, alisema mradi huo umewawezesha kutua mzigo mkubwa ambao hivi sasa wanaamini watoto hao watakuwa kama wenzao ambao siyo walemavu katika kupata mahitaji mbalimbali ya msingi.





# Msako wanasa mifuko 30 pembejeo feki

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

ZAIDI ya mifuko 30 ya mbegu feki za mazao, imekamatwa wilayani Rungwe baada ya kufanyika operesheni kwenye maduka mbalimbali ya pembejeo za kilimo.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vicent Anney, alisema jana kuwa kikosi kazi kikiongozwa na yeye kilifanya msako wa kushtukiza kwenye maduka ya pembejeo za kilimo na kukamata mbegu feki zilizokwisha muda wake.

Alisisitiza kuwa operesheni hiyo inaendelea maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo na kwamba wanakaobainika watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Aliwaonya wauzaji wote wa pembejeo kuzingatia kanuni na sheria za nchi na kwamba ni kosa kuuza bidhaa zilizokwisha muda wake kwani zinahatarisha afya za watumiaji.

"Operesheni kamata pembejeo feki bado inaendelea. Niwashauri tu wauzaji wa pembejeo za kilimo kuzingatia sheria maana tukikamata unashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Vilevile wakulima nawaasa acheni kuficha taarifa za mnaowajua wanauza mbegu zilizokwisha muda wake," alisema Dk. Anney.

Dk. Anney pia aliwashauri wakulima katika msimu huu wa kilimo kuhakikisha wanapanda mbegu bora ambazo zitahimili mabadiliko ya tabianchi.

Alisema wakulima wanatakiwa kupanda mazao yanayokomaa muda mfupi ili kukabiliana na uhaba wa mvua kwa sasa ambao kwa mujibu wa watabiri wa hali ya hewa walisema msimu huu wa kilimo kutakuwa na mvua chache.

Vilevile aliwasisitiza maofisa ugani kuendelea kuwatembelea wakulima maeneo yao ili kulima kilimo chenye tija badala ya kulima kwa mazoea ambapo huwatia hasara wakulima.

"Kama tulivyotaarifiwa na wataalamu wetu wa hali ya hewa msimu huu mvua si nyingi, mnapaswa kupanda mbegu bora za kilimo, lakini mwangalie mazao ambayo yanakomaa muda mfupi ili mwendane na hali ya sasa," alisema Dk. Anney.

Aliwahamasisha wawekezaji wa pembejeo za kilimo hususani wazalishaji wa mbolea kuendelea kuzalisha kwa wingi ili kukidhi mahitaji ya wakulima na kupunguza mfumuko wa bei.



Mkurugenzi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Nyasa, Elice Englibeth (kulia), akizungumza na wadau na viongozi mbalimbali wakati wa kikao cha uzinduzi wa mpango wa usimamizi jumuishi na uendelezaji wa raslimali za maji, jijini Mbeya juzi.
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wanafunzi 9,700 kuanza sekondari kwa kukamilika ujenzi wa madarasa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAFUNZI 9,713, waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wanatarajiwa kuanza masomo Januari 17, mwaka huu, baada ya kukamilika kwa asilimia 100 ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'anidako, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe juu ya maandalizi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2022.

Alisema serikali ilitoa Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya kujenga madarasa 92 na kutakiwa kukabidhi ifikapo Desemba 31, mwaka jana na kwamba walikamilisha kwa wakati kama ilivyoagizwa.

Alifafanua katika ya madarasa hayo 92, manane yanajengwa ghorofa moja kwenye Shule ya Sekondari ya Ruanda na kwamba ujenzi umefikia hatua za mwisho.

Mkurugenzi huyo alisema kwa idadi hiyo ya wanafunzi kulikuwa kunahitajika vyumba 243 vya madarasa na kwamba vilivyokuwapo ni 150 vyenye uwezo kuchukua wanafunzi 6,033.

Aliongeza kuwa kutokana na takwimu hizo wanafunzi 3,680 ndio walikuwa wanahitaji vyumba vya madarasa hivyo kukamilika kwa vyumba 92 kutasaidia kumaliza kabisa tatizo la uhaba wa madarasa kwa shule zote za sekondari jijini Mbeya.

"Halmashuari ya Jiji la Mbeya ilipokea Sh. bilioni 1.8 za UVIKO-19 zilizotolewa na serikali kujenga vyumba vya madarasa ili kukabiliana na uhaba wa madarasa tulipewa maelekezo na tulijitahidi kwa uwezo wetu na kuwa kinara wa halmashauri iliwahi kumaliza ujenzi vyumba vyote 92 vilivyohitajika," alisema Ng'anidako.

Pia Ng'anidako aliwasisitiza wazazi kuhakikisha watoto wote waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza kuwapeleka shule ili kupata haki zao za msingi na kutimiza ndoto kupitia elimu.

Alisema serikali imejenga miundombinu rafiki kwa ajili ya watoto kupata elimu kwa kuzingatia makundi yote na kuwasisitiza mabinti kujiepusha na makundi maovu ambayo yanaweza kuharibu ndoto zao.

# Tanzania sasa kuuza mafuta ya kupikia nje

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UTAFITI umeonyesha kuwa Tanzania itaanza kuuza mafuta ya kupikia nje ya nchi kutokana na ongezeko la eneo linalofaa kwa kilimo cha chikichi na matumizi ya mbegu bora kwa wakulima wa zao hilo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema hayo juzi wakati akikagua kitalu cha mbegu bora za chikichi ambazo zinaandaliwa kwa ajili ya kuwagawia wakulima wa zao hilo wilayani Kyela.

"Tumefanya utafiti na kupima udongo na kugundua kuwa kuna maeneo ambayo kutaongezeka uzalishaji wa zao la chikichi tafiti zetu zikikamilika tunaanza kupanda katika maeneo hayo. Naamini itakuwa mwarobaini wa kumaliza tatizo la uhaba wa mafuta nchini," alisema Dk. Bucheyeki.

Baadhi ya wakulima wa chikichi wilayani Kyela, waliiomba serikali kuendelea kuwasaidia katika suala la upatikanaji wa mbegu bora, ili kukidhi mahitaji yao na hatimaye waongeze uzalishaji wa mawese.

Miongoni mwa wakulima hao, Ibrahim Lameck, alisema wanahitaji kusaidiwa zaidi upatikanaji wa mbegu kwa sababu sasa Wanakyela wanachangamkia fursa hiyo ya kilimo cha michikichi kwani kinalipa ukilinganisha na zamani.

Alisema zao la chikichi linaingiza fedha nyingi kwa sababu kuanzia mbegu, mafuta na pumba zake vyote vinauzika na kuingiza hela tofauti na mazao mengine.

"Tunaomba ugawaji wa mbegu za chikichi uwafikie wakulima wote wa wilaya ya Kyela kwa sababu zikisambazwa kila eneo uzalishaji utaongezeka na hatimaye kuwa zao kuu la uchumi wilayani Kyela," alisema Lameck.

Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Kyela, Bernard Libata, alisema kutokana na ushirikiano uliopo baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na TARI Uyole, wakulima wana uhakika wa kupata mbegu bora za kutosha.

Alisema awamu ya kwanza wamefanya vizuri katika kuwapatia mbegu wakulima na kwamba wanaendelea na uzalishaji wa miche mingine ili kuwapatia wakulima.



## Waziri: Kilimo mazao Bahari ni dira ya SMZ

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Said Omar Shaaban, amesema kilimo cha mazao ya baharini ni sehemu ya mikakati ya Dira ya Maendeleo ya 2050 ambayo imelenga kuwainua wakulima wa mazao ya baharini katika uchumi wa bluu.

Akizindua mradi wa ufugaji wa majongoo ya pwani huko Fungu Refu, mkoa wa Kaskazini Unguja jana, alisema serikali imedhamiria na kujikita katika kilimo cha mazao ya baharini yakiwamo majongoo, mwani na ufugaji wa samaki na kaa ili kubadilisha maisha ya wananchi.

Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema imejipanga na kuweka vipaumbele vya kuwaendeleza wananchi katika sekta ya uchumi wa bluu na uvuvi wa bahari kuu.

Alisema kupitia fedha za ahuweni ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO- 19 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), serikali imekamilisha taratibu za ujenzi wa mabwawa 100 ya ufugaji wa majongoo ili kupatiwa wananchi wa wilaya zote za Unguja na Pemba ambayo yatawekwa miundombinu ya kisasa na vifaranga vya majongoo hayo.

Waziri aliwataka wakulima wa mazao ya baharini kuchangamkia fursa hizo kutokana na majongoo ya baharini kuwa na kipato kikubwa cha fedha kutokana na bei yake katika soko la kimataifa pamoja na matumizi mengi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu imejipanga kikamilifu kuwaendeleza wavuvi wa mazao ya baharini kwa ajili ya kupata kipato kikubwa katika uvuvi wa majongoo, kilimo cha mwani pamoja na samaki na kaa," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, akitoa taarifa ya kitaalamu kuhusu uzalishaji wa mazao ya baharini, alisema biashara ya majongoo bahari ilianza karne nyingi duniani ingawa kwa upande wa Zanzibar iliingia mwaka 1960 na kufanywa kienyeji zaidi huku wafanyabiashara na wanunuzi wakubwa wakiwa jamii ya Wachina waliopo nchini.

Alisema kutokana na kuongezeka kwa biashara hiyo zaidi katika nchi za bara la Asia hususani Singapore, China Japan, mashirika ya kimataifa yanayojishughulisha na uhifadhi wa mazingira ya baharini yamekuja na mbinu mpya za ufugaji wake ili kuwa bidhaa endelevu.

# Mbio kumrithi Maalim Seif zaanza

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANACHAMA wawili wa Chama cha ACT-Wazalendo akiwamo mwanasiasa mkongwe Tanzania, Juma Duni Haji, wamechukua fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa chama hicho, kumrithi Hayati Maalim Seif Sharif Hamad.

Uchukuaji wa fomu umefanyika kwa nyakati tofauti katika ofisi za chama hicho, Vuga mjini Zanzibar huku mwanachama wa pili aliyechukua fomu akiwa Hamad Masoud ambaye alishawahi kuwa Waziri wa Mawasiliano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Akizungumza baada ya kuchukua fomu hiyo, Duni alisema umri mkubwa alio nao si kigezo cha kushindwa kugombea nafasi hiyo kwa sababu akili yake iko vizuri na ana uwezo wa kukiongoza chama kupitia nafasi hiyo endapo atachaguliwa.

"Licha ya kwamba naitwa babu kutokana na umri wangu mkubwa, suala la umri si hoja kwangu kwa sababu akili yangu bado nzuri, ina uwezo, mikiki ya ushindani na kujadili masuala yanayohusu haki, uzalendo na uadilifu," alisema.

Duni alisema miaka ni namba tu kwa sababu rais wa Marekani ana miaka 73, hivyo hoja ya umri isitumike kuwa ni sababu.

Aliwaambia vijana wa chama hicho kwamba Maalim Seif ameondoka duniani sasa ni zamu yake kukiongoza chama chenye umoja na mshikamano.

Pia alisema kuwa mwaka 2025 ACT inatarajia kuchukua dola hivyo akipata nafasi ya uenyekiti atashirikiana na viongozi wenzake jinsi ya kukabili ushindani wa vyama ili kuchukua serikali na kutimiza ahadi za kuwaletea wananchi maendeleo na kulinda utu, uzalendo na uadilifu katika kuendesha serikali.

Alisema ACT-Wazalendo ndicho chama pekee kinachokua kwa kasi na kinategemewa na Watanzania kuwa chama kikuu cha upinzani kwa sababu kinajenga hoja badala ya malumbano.

"Matumaini yangu ni kwenda kukiongoza chama ambacho kinawapa matumaini wananchi ambacho kitawasaidia," alisema.

Naye Hamad Masoud alisema kuwa endapo atapata nafasi hiyo ataendeleza siasa za Maalim Seif Sharif Hamad ambazo ni siasa za maridhiano.

Alisema kuwa Maalim Seif alikuwa mtu wa watu na ni utambulisho katika siasa za Tanzania, hivyo atahakikisha anaendeleza sifa zake ambapo uwezo huo anao.

"Nimekuwa na kumsoma Maalim Seif ni kiongozi wa watu, hivyo nimeshajitayarisha vya kutosha kuvaa viatu vyake," alisema.




Mwanachama wa Chama cha ACT-Wazalendo, Hamad Masoud (kushoto), akipokea fomu ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa chama hicho, ili kumrithi marehemu Maalim Seif Sharif Hamad, kutoka kwa mjumbe wa kamati ya uchaguzi taifa wa chama hicho, Mhene Said Rashid, Vuga, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri aeleza azma ya SMZ ujenzi wa miundombinu bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali itaendelea kujenga miundombinu bora ya elimu kwa mujibu wa mahitaji ya wanafunzi wanaoandikishwa shuleni.

Amesema kufanya hivyo kutasaidia kuwawekea wanafunzi mazingira bora ya masomo ili kufanya vizuri katika masomo yao na kuongeza wataalamu nchini.

Waziri Soraga aliyasema hayo jana wakati akizindua jengo la madarasa sita na ofisi mbili za walimu katika Shule ya Mtoni Kidatu, Wilaya ya Magharib A, Unguja ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Soraga aliwataka wazazi, walezi na wananchi wa maeneo hayo, wahakikishe wanailinda miundombinu hiyo na kuwafuatilia watoto wao katika kuhakikisha wanafanya vizuri katika masomo na kuwa wenye nidhamu na uzalendo. Alisema serikali itaendelea kutekeleza malengo ya Mapinduzi yaliyoleta uhuru na kuondoa ubaguzi kwa kuwapatia wananchi huduma muhimu ikiwamo elimu bure.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis Juma, alisema madarasa hayo yatapunguza msongamano wa wanafunzi madarasani kutoka wanafunzi 90 hadi 60.

Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A', Suzan Peter Kunambi, alisema wilaya yake bado ina uhitaji wa madarasa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi na kwamba kwa sasa darasa moja lina wastani wa wanafunzi 120 kwa baadhi ya shule.

Akisoma risala, mwalimu wa shule hiyo, Halima Seif Khamis, alisema shule ina idadi kubwa ya wanafunzi na takwimu zinaonyesha kuwa na wanafunzi 4,060 wakiwamo 354 wa maandalizi, 2,740 msingi na 966 wa sekondari.

Mwakilishi wa Jimbo la Mwera, Mihayo Juma Nhunga, alisema licha ya juhudi za serikali kujenga shule lakini bado jimboni humo, kunaupungufu wa madarasa zaidi ya 50 kwa shule zilizomo katika jimbo hilo kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP.117 R. E 2019)**
**OATHS AND STATUTORY DECLARATION ACT, (CAP 34 R;E 2019)**
**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**



BY THIS DEED, I, LUCIA JUMA KENGEZA, a Female an adult Christian, Phone No. 0652-870711, Residing at Singida and a citizen of Tanzania, DO HEREBY ABSOLUTELY renounce and abandon the use of my formally name of EVALIN JUMA KINGEZA and in lie therefore do assume as from the date hereof the name of LUCIA JUMA KENGEZA as my name in lieu of the said name EVALIN JUMA KINGEZA. And in pursuance of such change of name as aforesaid, I HEREBY DECLARE, that I shall be known at all times hereunder in all records, deeds and instruments in writing and in all actions, proceedings, and in all dealings and transactions upon all occasions whatsoever, use and sign the name of LUCIA JUMA KENGEZA. I FURTHER DECLARE that all transactions, certificates, deeds and commitments that I have done in the past by using my former name of EVALIN JUMA KINGEZA are valid. I HEREBY AUTHORISE and request all persons and authorities to designate and address me, in the name of LUCIA JUMA KENGEZA as my name instead of the name renounced.
IN WITNESS HEREOF I have hereunder signed my assumed name of LUCIA JUMA KENGEZA and have set my hand this 26 day of 11, 2021.

**SWORN at SAME by the said LUCIA JUMA KENGEZA**
**Who is known to me personally**
**Me by……..**
**The latter being known to me personally………………DEPONENT**
**This 26 day of 11, 2021.**
**BEFORE ME**

BEFORE ME
NAME
SIGNATURE
ADDRESS
DATE
COMMISSIONER FOR OATHS

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Mseleche Julius Kaondo anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Verossa yenye namba za usajili T. 158 DKD. Yeyote atakayeiona kadi hiyo apeleke taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo Mjini Bariadi. Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo, imetolewa December 25 /2021 katika kituo cha polisi cha Bariadi kwa namba: SIM/BAR/RB/180/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ANDREW ANDREW FERDINANDS anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 127 CGA – BAJAJ BOXER. Chassis namba MD2A21BY3KWB85018. Engine namba PFZWKA22679. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: IRI/IRI/RB/456554/2021.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**
**Usimamiz wa Mirathi Na. 2/2022**
**Katika Shauri la Mirathi ya**
**FRANK JOSEPH KINYONGE………………Marehemu**
**Wa Njombe**
**Katika shauri la maombi ya kumteua Msimamizi yaliyoletwa na**
**MARCIANA FRANK KINYONGE…………Mwombaji**
**TANGAZO KWA UMMA**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 01 Mwaka 2022 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu Maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
Zingatia: Endapo kuna yeyote mwenye au anayejua kuhusu uliko wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 5 Mwezi 1 Mwaka 2022.

HAKIMU MKAZI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA …114….2021**
**MDAI: ALLAN CHALE**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: ASIA AME**

**Kwa: ASIA AME**
**Ombi la mdai: ALLAN CHALE**

**Madai ya :Talaka na matunzo ya motto shs:50,000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 31 mwezi 01 mwaka 2022 saa8:30 asubuhi.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 31 mwezi 12 mwaka 2021.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

RAJABU KASIMU RAJABU ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI M590 BWT AINA YA SANLG. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: KAH/RB/TR/ 01/2022.

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. ……./2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RAJABU SHENKHAWA MAUNGU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA OMARY RAJABU MAUNGU**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 01 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 4 Mwezi 01 Mwaka 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KITUO JUMUISHI
HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA NDOA
DAR ES SALAAM

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Tupigie 0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# 400 wauawa DRC kwa siku 30

**Kinshasa,** DRC

UMOJA wa Mataifa (UN), umesema takriban watu 400 waliuawa kiholela Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Novemba, pekee.

Uchunguzi umeonyesha kwamba asilimia 10 ya mauaji hayo yalifanywa na vikosi vya usalama vya serikali.

Ofisi ya pamoja ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa Congo, imesema mwezi Novemba pekee mawakala wa serikali walihusika na mauaji ya kiholela ya watu 40, wakiwamo wanaume 24, wanawake tisa na watoto saba.

Ripoti hiyo ya UN, iliyotolewa juzi, ilisema kwamba wapiganaji wanaomiliki silaha, waliwaua watu wasiopungua 345, wakiwamo wanawake 61 na watoto 26 katika kipindi hicho cha mwezi mmoja.

"Mwezi Desemba hali ilikuwa mbaya zaidi."

Umoja wa Mataifa, uliorodhesha zaidi ya visa 800 vya ukiukaji wa haki za binadamu katika eneo lote la DRC, sawa na ongezeko la asilimia 61 ukilinganisha na mwezi mmoja kabla.

Juhudi za kuwapata viongozi wa DRC, kutoa maoni yao, kufuatia ripoti hiyo, hazikufua dafu.

Omar Kavota, mratibu wa Shirika la Kutetea Haki za Binadamu jimboni Kivu ya Kaskazini, CEPADHO, alisema takwimu hizo za UN, ni chini ya makadirio.

"Ripoti hii ya Umoja wa Mataifa ni ya kweli. Na pengine tukizingatia hali ya mambo ilivyo kwenye uwanja wa machafuko utakuta kwamba visa vya ukiukwaji wa haki za binadamu ni vingi kuliko hata Umoja wa Mataifa ulivyoripoti.

"Hiyo ni ripoti ya mwezi Novemba, ukitizama mwezi Desemba hali ilikuwa mbaya zaidi," alisema Kavota.

Kwa mujibu wa ripoti, visa vingi vya ukiukaji wa haki za binadamu vilifanyika jimboni Kivu ya Kaskazini, likifuatiwa na majimbo la Ituri, Tanganyika na Kivu ya Kusini.

Mikoa hiyo yote iko kwenye eneo la Mashariki mwa DRC.

Tangu Mei mwaka jana, mikoa ya Kivu Kaskazini na Ituri imekuwa chini ya uongozi wa kijeshi, kwa lengo la kukomesha shughuli za makundi yenye silaha.

Hatua hiyo ya kipekee iliyochukuliwa na Rais Felix Tshisekedi, imelipa jeshi mamlaka kamili kwenye mikoa hiyo, hadi sasa halijafanikiwa kuzuia mauaji yanayofanywa na makundi yenye silaha ambayo yamevuruga eneo hilo kwa miaka 25 sasa.

Makundi ya waasi yanayohusishwa na ukatili huo ni pamoja na wapiganaji wa ADF, kundi la Nyatura, waasi wa Rwanda wa FDLR na wapiganaji wa CODECO ambao ni kundi la kikabila, mkoani Ituri.

**DW**



Mwandamanaji akiwa amebeba ngao ya polisi mbele ya maofisa usalama, wakati wa maandamano mjini Almaty, nchini Kazakhstan, juzi. Rais wa Kazakhstan, Kassym Jomart Tokayev, ameomba msaada wa kijeshi Urusi, kukabiliana na maandamano yanayoendelea ya kuipinga serikali yake. **PICHA: AP**

## Pipi zamwondoa mbunge bungeni

**Nairobi,** KENYA

MBUNGE wa Kenya, amefurushwa kikaoni kwa siku moja baada ya kupatikana akigawa peremende kwa wenzake, wakati mjadala ulipokuwa unaendelea.

Fatuma Gedi, alifanya hivyo juzi, akidai alibaini viwango vya sukari vilikuwa vimeshuka, kutokana na kushiriki kikao kirefu.

Alikuwa anatuhumiwa na mbunge mwenzake, Ndindi Nyoro, kwamba alikuwa akigawa pesa ndani ya ukumbi wa bunge.

Nyoro, aliombwa kuthibitisha madai yake ya hongo na kuzuiliwa kuhudhuria vikao kwa siku mbili, kwa kosa hilo.

Gedi, pia alizuiliwa kuhudhuria kikao kimoja kwa kosa la kugawa peremende bungeni.

Wabunge waliidhinisha marekebisho kadhaa katika muswada wa vyama vya siasa, kabla ya uchaguzi mkuu, mwaka huu

**BBC**

## Marekani, Japan kuzungumza wiki hii

**New York,** MAREKANI

MAREKANI na Japan, zinatarajia kufanya mazungumzo kwa njia ya mtandao wiki hii, ambapo yatarejea ahadi zao za kulinda eneo la Indo-Pacific, ikiwa ni katikati ya kuongezeka kwa changamoto kutoka China na vitisho vya nyuklia na makombora kutoka Korea Kaskazini.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken na Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Austin Lloyd wamekutana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Japan, Yoshimasa Hayashi na Waziri wa Uinzi wa Japan, Nobuo Kishi, jana kwenye mkutano wa pamoja kwa njia ya mtandao.

Mkutano huo ulifanyika siku moja, viongozi wa Japan na Australia, wanatarajiwa kutia saini makubaliano mapya ya usalama, yakiwa na lengo la kuweka mkakati kwa mara ya kwanza, ili vikosi vya ulinzi vya mataifa hayo kufanya kazi pamoja.

Kutokana na hayo, Wizara ya Mambo ya Nje ya China, yenyewe imeonyesha wasiwasi kuhusu makubaliano ya kiusalama yanayofanyika baina ya Japan, Australia, India na Marekani.

**VOA**

# Papa: Upendo kwa wanyama badala ya watoto ni ubinafsi

**Vatican,** ROMA

PAPA Francis, amependekeza kwamba watu wanaochagua kuwapenda wanyama zaidi ya watoto, ni wabinafsi.

Papa alizungumza hayo alipokuwa akijadili kuhusu suala la uzazi, mjini Vatican.

"Leo tunaona aina tofauti ya ubinafsi. Tunaona baadhi ya watu hawataki kupata mtoto. Wakati wengine wana mtoto mmoja tu, lakini wana mbwa na paka, ambao huchukua nafasi ya watoto.

"Hii inaweza kufanya watu kucheka, lakini ndio uhalisia. Kitendo hicho ni kukataa kuwa baba na mama na kibaya, kinaondoa ubinadamu wetu," alieleza kiongozi huyo mkuu wa Kanisa Katoliki duniani.

Papa Francis, alisema kwamba watu ambao hawawezi kupata watoto kwa sababu za kibaiolojia wanapaswa kuzingatia kuasili na kuwataka watu wasiogope kuwa wazazi.

Pia alizungumzia juu ya msimu wa baridi huku idadi ya watu isiyotaka kupata watoto ikiongezeka, na kwamba watu hawataki kupata watoto zaidi na zaidi.

Si mara ya kwanza kwa Papa Francis kulenga watu wanaochagua kuwapenda wanyama badala ya watoto.

Mwaka 2014, alisema mapenzi na wanyama badala ya watoto, lilikuwa jambo jingine la uharibifu wa kitamaduni na kwamba uhusiano wa kihisia na wanyama ulikuwa rahisi, kuliko uhusiano kati ya wazazi na watoto.

**BBC**

# SIMBA YAWATAKA MASHABIKI KUTULIA, CHAMA KITAELEWEKA

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Simba umewataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kutulia na kutoyumbishwa kuhusiana na masuala mbalimbali ya usajili ukiwamo na wa aliyekuwa kiungo wao waliyemuuza Morocco, Clatous Chama.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema bado klabu hiyo inaendelea na mchakato wa usajili wa dirisha dogo na muda utakapofika wataweka hadharani majina ya wachezaji waliokamilisha usajili wao.

Salim alisema Simba haijawahi kushindwa kwenye vita yoyote ile ya mambo ya usajili kama ina nia thabiti ya kumtaka mchezaji husika anayewaniwa.

"Tunawataka wanachama na mashabiki wa Simba watulie, sisi viongozi wao tunafanya kazi bila majigambo wala kelele, mambo mazuri yanakuja. Hatujawahi kushindwa vita yoyote ile, hata iwe angani, tuko makini sana, na kazi yetu ni kuwapa wao furaha," alisema Salim.

Aliongeza subira ni muhimu katika kipindi hiki na hatima ya Chama ambaye ni mali ya RS Berkane itajulikana ndani ya muda mfupi ujao.

"Dirisha linafungwa Januari 15, mwaka huu, bado siku chache tu, msiwe na haraka, muda utaongea," alisema mwenyekiti huyo.

Alimtaja Msudan Sharaf Eldin Shiboub ni mchezaji mwalikwa tu kwa sababu aliomba kucheza michuano ya Kombe la Mapinduzi na si kufanya majaribio kama inavyozungumzwa, huku Cheick Moukoro raia wa Ivory Coast ambaye alivutia watu wengi dakika chache tu alizocheza kwenye mechi ya juzi dhidi ya Selem View yeye amekuja kwa majaribio.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema viongozi wako kwenye harakati za kumrejesha Chama, ingawa kama atarejea atashindwa kucheza michuano ya Kombe la Shirikisho kwani tayari alishaitumikia RS Berkane ambayo nayo imo kwenye michuano hiyo na timu hizo zikiwa kundi moja.




Kiungo wa Simba, Rally Bwalya (wapili kulia), akiwa ameshikilia mfano wa hundi ya Sh. 500,000 baada ya kutangazwa Mchezaji Bora wa mechi kati ya Simba dhidi ya Selem View iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar juzi. **PICHA: SIMBA SC**

# Hitimana, KMC FC wamalizana

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Msaidizi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Simba, Thierry Hitimana, amesaini mkataba wa mwaka mmoja wa kukinoa kikosi cha KMC FC cha jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Ujio wa Hitimana ndani ya timu hiyo umewaondoa makocha wawili waliokuwapo, Habib Kondo na John Simkoko.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana Mwenyekiti wa Bodi ya KMC FC, Songoro Mnyonge, alisema wamefikia uamuzi wa kufanya mabadiliko ya benchi baada ya kujitathmini na kuona mapungufu yao.

Mnyonge alisema licha ya kusajili wachezaji wazuri, lakini timu haikuwa na matokeo chanya na hivyo wakabaini mapungufu yalikuwa kwenye benchi la ufundi.

"Tumekaa na kutafakari madhaifu yetu yalikuwa katika masuala ya kiufundi na kimbinu, na sio wachezaji, uamuzi wa kumchukua Hitimana ambaye tunaimani na utendaji wake wa kazi kutokana na timu alizopita," alisema kiongozi huyo.

Naye Hitimana alisema amekubali kutua KMC baada ya kufikia makubaliano na anaamini atahakikisha anaiboresha timu hiyo ili irejee katika ubora wake.

"Naifahamu vyema Ligi ya Tanzania, nina imani kwa uwezo wangu nitajitahidi kuhakikisha tunaenda vizuri na kusaidia timu hii kurejea katika ubora wake," alisema Hitimana.

## Msemaji Simba awataka Yanga

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya timu yake kuanza vyema mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Ofisa Habari na Mawasiliano mpya wa Simba, Ahmed Ally, amesema mchezo dhidi ya Selem View ilikuwa ni njia tu ya kuwapeleka hatua inayofuata kwenye michuano hiyo.

Simba ilianza michuano hiyo kwa ushindi wa mabao 2-0 na leo itashuka dimbani tena kucheza dhidi ya Mlandege kutoka visiwani hapa.

Katika mchezo huo, nyota wa kimataifa wa timu hiyo kutoka Zambia, Rally Bwalya, alitangazwa kuwa Mchezaji Bora wa mechi na kukabidhiwa kitita cha Sh. 500,000 kutoka kwa wadhamini wa zawadi hiyo, Shirikia la Bima Tanzania (NIC).

Ally alisema timu yao imejipanga vizuri kuhakikisha inalichukua kombe la michuano hiyo kwa mwaka huu na ushindi wa juzi ni ishara ya kuelekea kwenye malengo yao.

"Niseme Selem View ilikuwa ni njia tu yakupita, ila kuna watu tunawataka na wamekuja na kombe huku Zanzibar, hao ndio walengwa wetu wakubwa," Ally alisema.

Aliongeza kwa kuwapongeza wachezaji wao kwa kuonyesha kiwango kizuri dhidi ya Selem View ambao nao walionyesha uwezo wa kumiliki mpira pale walipokuwa nao.

## Serikali yawaonya mapromota 'feki'

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limetoa onyo kali kwa viongozi wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Nchini (TPBRC), ambao walihusika katika mchakato wa kutoa kibali kwa bondia Mghana, Richard Lartey, kupigana kwa kutumia leseni iliyotolewa Tanzania.

Novemba 3, mwaka jana, Lartey alienda kupambana Urusi kwa kutumia kibali kutoka Tanzania kufuatia kufungiwa na mamlaka ya mchezo huo kwao Ghana.

Viongozi hao waliopewa onyo ni Makamu wa Rais wa TPBRC, Agapito Jambalaya na Katibu wake, Yahya Poli.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa BMT, Najaha Bakari, alisema viongozi hao wanatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia taratibu na kuacha kufanya uamuzi ambao unalichafua taifa.

Alisema BMT inawataka mapromota, mawakala na viongozi wa vyama vya michezo vyote kuhakikisha wanazingatia taratibu, mwongozo, kanuni na sheria zinazosimamia michezo nchini.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**ORIGI ATAKIWA LAZIO**
MKURUGENZI wa Michezo wa Lazio, Igli Tare, ameanzisha mazungumzo na Liverpool kumhusu mshambuliaji wa Ubelgiji, Divock Origi, huku wekundu hao wakiwa tayari kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa kuhofia kumpoteza kwa uhamisho wa bure ifikapo Juni, mwaka huu. ***(LazioNews24)***

**NEVES ANUKIA UNITED**
KLABU ya Manchester United imedhamiria kumsajili kiungo wa Wolverhampton Wanderers na Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Neves mwenye miaka 24, katika dirisha la usajili lililofunguliwa mwezi huu. ***(The Sun)***

**GERRARD AMTAKA COUTINHO**
KOCHA wa Aston Villa, Steven Gerrard amempigia simu binafsi kiungo wa kati wa Barcelona, Philippe Coutinho, ambaye alicheza naye Liverpool, kuhusu uwezekano wa Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 29 kuhamia Villa Park kwa mkopo. ***(El Partidazo de Cope, via Mirror)***

**WILLIAMS, PHILLIPS WAJIPANGA**
LIVERPOOL huenda ikamruhusu mlinzi wa Wales, Neco Williams, mwenye miaka 20, na beki wa Mwingereza, Nathaniel Phillips (24), kuondoka katika klabu hiyo katika dirisha la uhamisho wa Januari. ***(Sky Sports)***

**RAMSEY KUONDOKA JUVE**
KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Wales, Aaron Ramsey mwenye miaka 31, anajiandaa kuondoka Juventus, ambako analipwa mshahara wa euro 325,000 kwa wiki. ***(Sky Sports)***

**DIGNE NJIA MOJA**
KIUNGO wa Everton, Lucas Digne mwenye umri wa miaka 28, huenda akahamia klabu nyingine ya Ligi Kuu England. Hata hivyo Newcastle United sio chaguo la mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa. ***(Fabrizio Romano via Twitter)***

**DEST KUMRITHI DIGNE**
CHELSEA wanatafakari uwezekano wa kumnunua beki wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21, kama mbadala wa Lucas Digne. ***(Daily Star)***


**UMTITI KUTUA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle wamepewa beki wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Samuel Umtiti mwenye umri wa miaka 28 na Barcelona kwa mkataba wa mkopo na chaguo la kumnunua kwa mkataba wa kudumu hapo baadaye. ***(Daily Mail)***

**VILLA KUMKOSA GOMEZ**
ASTON Villa hawana 'nafasi' ya kumsajili kiungo wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Joe Gomez. ***(Athletic)***

**HATIMA YA HAALAND YAJA**
KLABU ya Borussia Dortmund watafanya uamuzi kuhusu hatima ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Norway mwenye umri wa miaka 21, Erling Braut Haaland 'wiki chache zijazo'. ***(Daily Mail)***

**WEST YAMWANIA BARBOSA**
KLABU ya West Ham wamewasilisha dau la pauni milioni tano la kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Flamengo, Mbrazil Gabriel Barbosa mwenye miaka 25, hadi Desemba 2023. ***(Sport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA YAJITOSA KUMSAJILI CAVANI

**Ni baada ya vigogo hao wa Hispania kukosa nafasi ya kumpata Morata ambaye...**

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona inamhitaji mshambuliaji wa klabu ya Manchester United, Edinson Cavani, kwenye dirisha hili la Januari baada ya Juventus kuthibitisha Alvaro Morata haendi popote.

Baada ya kocha wa Barcelona, Xavi kushindwa kunasa saini ya Morata, sasa amehamia kwenye 'mpango mwingine' wa kutaka kumpata mshambuliaji huyo ambaye ataweza kuchukua nafasi ya Sergio Aguero aliyestaafu hivi karibuni.

Ingawa Barcelona wana kipindi kigumu kwenye usajili, lakini wamepanga kupunguza wachezaji wote wenye mishahara mikubwa.

Hiyo ni kwa ajili waweze kupata nafasi ya kusajili wachezaji wapya, huku wengine wakiwa wamefunguliwa milango ya kuondoka.

Baadhi ya nyota ambao Barca imewafungulia milango ya kujiunga na timu nyingine ni pamoja na Philippe Coutinho na Samuel Umtiti.

Ingawa anahitajika na Barcelona, Cavani muda anaopewa kucheza ndani ya Manchester United ni mdogo, lakini bado ni mchezaji muhimu kwenye kikosi cha Mashetani Wekundu ambacho kwa sasa kiko chini ya kocha wa muda, Ralf Rangnick.

MECHI KALI
HOME
BAYERN MUNCHEN
1.38 | 5.57 | 6.17
MONCHENGLADBACH
AWAY
KUWEKA PESA:
vs PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
vs WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 823



# RONALDO AZUA BALAA UNITED

**MANCHESTER, England**

KUREJEA kwa Cristiano Ronaldo ndani ya Manchester United kumeripotiwa kuzua mvutano katika kikosi cha kwanza, huku Kocha Mkuu wa muda, Ralf Rangnick akishughulikia mgawanyiko kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

Mashetani Wekundu hao walipokea kichapo cha 1-0 kutoka kwa Wolverhampton Wanderers kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa Jumatatu, na Luke Shaw alibainisha kikosi kimekosa umoja.

Kwa mujibu wa The Express, Harry Maguire, Edinson Cavani na Mason Greenwood ni miongoni mwa wachezaji ambao wanaona kurejea kwa Ronaldo ni changamoto kwa majukumu yao yanayotarajiwa, huku pia kukiwa na wasiwasi juu ya ushawishi wa mshambuliaji huyo kwa wachezaji wanaozungumza Kireno katika klabu hiyo.

Ripoti hiyo inadai chumba cha kubadilishia nguo kimekua na mgawanyiko wa vikundi vidogo vidogo, huku timu ikijitahidi kuimarisha mshikamano, kutokana na lawama zilizolengwa kwa wachezaji na nahodha wa zamani wa klabu hiyo, Gary Neville baada ya sare ya 1-1 dhidi ya Newcastle United hapo Desemba 27, mwaka jana.

Ronaldo amefunga mabao 14 katika mechi 21 alizoichezea United tangu arejee katika klabu hiyo, yakiwamo magoli nane katika mechi 16 za Ligi Kuu England.

# Ramsey ajiandaa kurejea England

**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus amefungua milango kwa, Aaron Ramsey kuondoka katika klabu hiyo mwezi huu.

Hivi karibuni Ramsey amekuwa akihusishwa na klabu mbalimbali za England ikiwamo timu zake za zamani, Arsenal, Everton na Newcastle United.

Jumanne iliripotiwa klabu ya Burnley ilipeleka rasmi ofa kwa mchezaji huyo na kukataliwa na Ramsey mwenyewe.

Taarifa za kuondoka kwake zimekuwa zikiongezeka mwezi huu kutokana na ukweli hana nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha Juve.

Ramsey alijiunga na Juventus akiwa mchezaji huru akitokea Arsenal majira ya joto mwaka 2019.



## HABARI MICHEZO


...,998,440

JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 9/1/22 | 16:30 | Cagliari vs Bologna | 3.15 | 3.30 | 2.27 |
| 2. 9/1/22 | 16:30 | Torino vs Fiorentina | 2.56 | 3.41 | 2.66 |
| 3. 9/1/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Reims | 2.42 | 3.14 | 2.99 |
| 4. 9/1/22 | 17:30 | Hertha BSC vs FC Koln | 2.66 | 3.46 | 2.51 |
| 5. 9/1/22 | 19:05 | Nantes vs Monaco | 3.22 | 3.27 | 2.23 |
| 6. 9/1/22 | 20:15 | Malaga vs Sporting Gijon | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 7. 9/1/22 | 20:30 | Alaves vs Athletic Bilbao | 3.25 | 3.05 | 2.35 |
| 8. 9/1/22 | 20:30 | Roma vs Juventus | 3.07 | 3.31 | 2.31 |
| 9. 9/1/22 | 20:30 | Genoa vs Spezia | 2.28 | 3.29 | 3.14 |
| 10. 9/1/22 | 22:30 | Ponferradina vs Zaragoza | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 11. 9/1/22 | 23:00 | Villarreal vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 9/1/22 | 23:30 | Las Palmas UD vs Almeria | 2.76 | 3.05 | 2.56 |
| 13. 9/1/22 | 23:30 | Belenenses vs FC Arouca | 2.57 | 3.02 | 2.82 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 07 - JANUARI 2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 5532 | Rayka Babol vs Kheybar Khorramabad FC | 3.71 | 2.70 | 2.17 |
| 14:00 | 3673 | Lusaka Dynamos vs Green Buffaloes | 4.43 | 3.08 | 1.82 |
| 15:00 | 1120 | Express FC vs Bright Stars | 1.23 | 5.43 | 9.69 |
| 15:00 | 2594 | Gaddafi FC vs Wakiso Giants FC | 2.47 | 3.14 | 2.66 |
| 15:20 | 3219 | AL Baten vs Al-Ettifaq | 2.53 | 3.32 | 2.68 |
| 15:50 | 4264 | Muscat Club vs Al Nahda (Oman) | 3.38 | 3.24 | 2.02 |
| 15:55 | 1035 | AL Musanaa vs Oman Club | 1.69 | 3.48 | 4.54 |
| 15:55 | 1650 | Saham Club vs Nizwa | 1.92 | 3.31 | 3.60 |
| 15:55 | 5162 | Bahla vs Al Seeb | 4.62 | 3.42 | 1.69 |
| 16:00 | 2330 | Hapoel Acre vs Hapoel Raanana | 2.13 | 3.12 | 3.57 |
| 16:00 | 2540 | Ahi Nazareth vs El Fahem | 3.03 | 3.08 | 2.41 |
| 16:00 | 4586 | Beitar Tel Aviv Ramla vs Hapoel Kfar Saba | 3.41 | 3.21 | 2.15 |
| 16:00 | 4587 | Hapoel Rishon Lezion vs Bnei Yehuda | 5.34 | 3.51 | 1.67 |
| 16:00 | 5338 | Zanaco vs Kansanshi Dynamos | 2.04 | 2.93 | 3.74 |
| 16:00 | 5419 | Hapoel Ramat Gan vs AS Ashdod | 2.17 | 3.21 | 3.36 |
| 16:15 | 2335 | Al-Sailiya SC vs Al-Shamal | 2.25 | 3.48 | 2.71 |
| 16:20 | 2032 | Dhofar Salalah vs Sohar Club | 1.30 | 4.80 | 8.26 |
| 17:00 | 1263 | Paradou AC vs RC Arbaa | 1.32 | 4.43 | 8.66 |
| 17:00 | 3531 | CS Constantine vs JS Saoura | 1.82 | 3.18 | 4.24 |
| 17:00 | 4373 | CR Belouizdad vs JS Kabylie | 1.57 | 3.52 | 5.59 |
| 17:00 | 5502 | MC Alger vs US Biskra | 1.63 | 3.70 | 5.60 |
| 17:00 | 5606 | East Bengal vs Mumbai City FC | 5.21 | 4.43 | 1.47 |
| 18:00 | 1853 | Cfc-Cf Canelas 2010 vs AD Fafe | 2.25 | 3.18 | 2.94 |
| 18:00 | 5568 | Puebla U20 vs America Mexico U20 | 2.55 | 3.32 | 2.46 |
| 18:05 | 2909 | Al Taawon vs AL Hazm | 1.70 | 3.81 | 4.55 |
| 18:25 | 2227 | Al Sadd SC vs Qatar SC | 1.14 | 7.13 | 12.52 |
| 18:25 | 3568 | Al Gharafa SC vs Al Ahli Doha SC | 1.91 | 3.51 | 3.42 |
| 19:00 | 2720 | Al Suwaiq vs Rustaq Club | 2.64 | 3.12 | 2.50 |
| 19:00 | 5803 | FC Juarez U20 vs Necaxa U20 | 2.74 | 3.32 | 2.31 |
| 19:55 | 2322 | Al Ittihad Jeddah vs AL Faiha | 1.66 | 3.76 | 4.95 |
| 20:00 | 2474 | Trabzonspor vs Yeni Malatyaspor | 1.36 | 4.72 | 7.87 |
| 20:00 | 5475 | MC Oran vs ASO Chlef | 1.99 | 3.12 | 3.61 |
| 20:30 | 1584 | Avranches vs Le Mans | 2.70 | 3.04 | 2.60 |
| 20:30 | 2613 | Saint Brieuc vs Boulogne | 2.49 | 2.93 | 2.93 |
| 20:30 | 3163 | Annecy FC vs Bourg Peronnas | 2.21 | 2.98 | 3.37 |
| 20:30 | 3395 | Red Star vs Laval | 2.18 | 3.08 | 3.32 |
| 20:30 | 4072 | Orleans vs Sedan | 2.00 | 3.28 | 3.57 |
| 20:30 | 4153 | Chambly vs Concarneau | 3.33 | 3.08 | 2.17 |
| 20:30 | 4794 | Villefranche Sur Saone vs Sete 34 FC | 1.49 | 4.02 | 6.07 |
| 20:30 | 5702 | Bastia Borgo vs Chateauroux | 3.66 | 3.17 | 2.01 |
| 20:45 | 4437 | Helmond Sport vs Dordrecht | 1.68 | 4.09 | 4.09 |
| 21:30 | 3150 | Santa Clara vs Sporting Lisbon | 8.08 | 4.53 | 1.37 |
| 22:30 | 1323 | Bayern Munchen vs Monchengladbach | 1.38 | 5.57 | 6.17 |
| 22:30 | 3841 | Exeter vs Portsmouth | 3.27 | 3.37 | 2.01 |
| 22:30 | 5703 | U.Leiria vs Cova da Piedade | 1.29 | 4.62 | 9.24 |
| 22:45 | 2097 | Edinburgh City vs Elgin City | 2.33 | 3.19 | 2.80 |
| 23:00 | 1001 | Swindon Town vs Manchester City | 23.91 | 8.76 | 1.09 |
| 23:00 | 2579 | Amorebieta vs Tenerife | 3.44 | 3.14 | 2.12 |
| 23:00 | 2689 | Roda Kerkrade vs Maastricht | 1.23 | 6.26 | 8.80 |
| 23:00 | 3296 | Bordeaux vs Marseille | 5.59 | 4.39 | 1.52 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NKANE AKITAKA KIATU CHA DHAHABU, AMTAJA NGASA

**Na Adam Fungamwango**

WINGA mpya wa Yanga, Dennis Nkane, amesema kufananishwa na nyota wa zamani wa timu hiyo, Mrisho Ngasa kwake ni heshima kubwa, hivyo amejiandaa 'kuvaa viatu' vya nyota huyo, lakini akitarajia kuweka rekodi mbalimbali klabuni hapo.

Nkane amesema hayo baada ya kuonyesha kiwango kizuri katika mechi yake ya kwanza akiwa na Yanga juzi na kufunga bao moja kwenye ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Taifa Jang'ombe kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayofanyika Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili, Nkane alisema lengo lake ni kujituma zaidi na anatarajia kuvunja rekodi mbalimbali zilizowekwa ndani ya klabu hiyo.

Nkane ambaye amejiunga na Yanga akitokea Biashara United amesema anawataka wanachama na mashabiki wa Yanga watarajie mazuri mengi kutoka kwake.

"Kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa kujiunga na klabu kubwa kama Yanga na kuvaa jezi hii, ni furaha yangu kubwa na kuona nafunga kwenye mchezo wangu wa kwanza nikiwa na klabu hii na huu ni mwanzo tu, matarajio yangu ni mengi mazuri yatakuja," alisema mchezaji huyo chipukizi.

Alisema hana wasiwasi wa kukosa namba kwenye timu hiyo na anadhani uwepo kwa wachezaji kama Fiston Mayele, Heritier Makambo, Jesus Moloko pamoja na yeye kutaisaidia Yanga kufanya vyema kwenye kampeni yake ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano mengine wanayoshiriki.

Nkane alisema kupewa namba 16 aliyokuwa akiivaa Ngasa ni jambo la fahari kwake ambapo ametambuliwa na kukubalika kama alivyokuwa mkongwe huyo, hivyo hatomwangusha na anahidi kuweka rekodi zake zote na hata kuzidi hapo.

"Kwanza kabisa nataka niwe mmoja wa wanaowania ufungaji bora kwenye Ligi Kuu na kuisaidia Yanga ubingwa msimu huu, halafu mengine yatafuata," Nkane alisema.



Winga mpya wa Yanga, Dennis Nkane (kushoto), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Taifa Jang'ombe katika mechi ya michuano ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## Odhiambo kocha mpya Prisons

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Tanzania Prisons umeingia mkataba wa mwaka mmoja na Mkenya Patrick Odhiambo kwa ajili ya kukinoa kikosi cha timu hiyo kinachoshiriki Ligi Kuu Bara.

Odhiambo ametua Tanzania Prisons akitokea Biashara United, baada ya Salum Mayanga kuachana na timu hiyo na kurejea Mtibwa Sugar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Tanzania Prisons, Mkwanda Mkwanda, alisema wameingia mkataba na Odhiambo kwa ajili ya kurejesha makali ya timu yao ambayo msimu huu imeanza vibaya.

Mkwanda alisema baada ya kupitia nakala za makocha mbalimbali walioomba kazi waliamua 'kuangukia' kwa kocha huyo wa kigeni kwa sababu anaifahamu vyema Ligi Kuu Bara.

"Tunaimani na Odhiambo kufikia mikakati yetu ya kuendelea kufanya vizuri katika ligi na kurejesha ubora wetu wa misimu iliyopita kuwa tishio kwa timu kubwa," alisema Mkwanda.

Aliongeza baada ya kumalizana na Odhiambo huku mchakato unaofuata ni kuboresha kikosi chao kwa kusajili wachezaji wapya watakaoisaidia timu kufikia malengo.

"Mazungumzo yameenda vizuri na wachezaji hao ambao ni Mudathir Abdallah (Coastal Union) na Abubakar Malika (Mwadui FC), wote ni washambuliaji," alisema Mkwanda.

Michezo
Ijumaa Januari 7, 2022
Nipashe



## Barca yajitosa kumsajili Cavani



Winga wa Yanga, Deus Kaseke (kushoto), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Taifa Jang'ombe katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YATAMBA IMELAMBA DUME

### Kaze asema watashusha kikosi kamili kuikabili KMKM ili...

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI Yanga inatarajia kuvaana na 'Maafande' wa KMKM katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Mapinduzi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Cedrick Kaze, amesema wamefurahishwa na viwango vya nyota wao wapya.

Yanga itawakabili KMKM kuanzia saa 10:15 jioni na endapo itaibuka na ushindi katika mchezo huo, itaongoza Kundi B na kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze, alisema wachezaji wapya waliojiunga na timu hiyo katika dirisha dogo la usajili lililofunguliwa hivi karibuni wameanza vizuri na anaamini wataingia katika 'mfumo' wa timu yao ndani ya muda mfupi.

Kocha huyo alisema licha ya kufanya mazoezi ya pamoja na wenzao kwa siku moja, nyota hao wapya wameonyesha ubora uliowafanya wasajiliwe ndani ya kikosi hicho kinachotetea ubingwa wa mashindano hayo.

"Wamecheza vizuri, licha ya kufanya mazoezi kwa siku chache na wenzao ambao wapo pamoja karibu miezi minne, wengine miezi miwili, lakini wameonyesha kuungana vyema, ni dalili njema kwao," alisema Kaze.

Aliongeza wapinzani wao pia walikuwa na kikosi kizuri na kilionyesha ushindani lakini ubora wao uliwafanya waibuke na ushindi katika mechi hiyo ya kwanza dhidi ya Taifa Jang'ombe iliyomalizika kwa ushindi wa mabao 2-0.

"Taifa Jang'ombe ina kikosi kizuri, walionyesha upinzani, walifanya vizuri katika dakika za mwanzoni ikiwamo kuziba njia zote, wana wachezaji vijana wenye mbio, isipokuwa makosa madogo madogo ndio yametupa nafasi sisi tukazitumia vyema, ila walipambana," aliongeza Kaze, kocha huyo raia wa Burundi.

Kuelekea mchezo wao wa leo dhidi ya KMKM, Kaze, alisema wamejipanga kuhakikisha wanaendelea kutoa 'dozi' ili wapate tiketi ya kusonga mbele katika michuano hiyo na hatimaye kufikia malengo yao ya kutetea ubingwa wanaoushikilia.

"Natumaini wachezaji wangu watacheza vizuri zaidi katika mechi ya kesho (leo), tutakuwa na kikosi kilichokamilika, wachezaji ambao hawakuonekana katika mechi ya kwanza, lengo ni kufanya vizuri na kutetea ubingwa," aliongeza Kaze.

Alisema wamejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu wapinzani wao KMKM hawatakuwa na presha yoyote kutokana na wao wana nafasi ya kusonga mbele katika mashindano haya.

Naye Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na wamejiandaa kuhakikisha wanaondoka na matokeo chanya na kuiwakilisha vyema Zanzibar kwenye kinyang'anyiro cha kuwania taji.

Msimu alisema anaiheshimu Yanga lakini katika mechi ya leo wasitarajie mteremko kutokana na tayari wameshafahamu ubora wa udhaifu wa kikosi chao.

"Kikubwa lolote linaweza kutokea japo mimi matarajio yangu ni kupata ushindi, malengo yetu mwaka huu ni kunyakuwa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, tulianza maandalizi mapema kupitia mechi za Ligi Kuu Zanzibar," alisema Msimu.

Mechi nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Simba dhidi ya Mlandege wakati hatua ya makundi itamalizika kesho kwa Azam FC kuwakabili Yosso Boys.

## Simba SC kuikabili Mlandege kibabe

**Na Saada Akida**

LOLOTE linaweza kutokea huko mbele. Ni kama Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, ameanza kukiandaa kisawasawa kikosi chake kwa kulifanyia kazi tatizo la upigaji penalti katika timu yake inayoshiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea huko Zanzibar.

Simba itashuka kuwakabili Mlandege katika mchezo wake wa mwisho wa Kundi C utakaochezwa kuanzia saa 2:15 usiku kwenye Uwanja wa Amaan.

Pablo aliliambia gazeti hili ameshapata 'dawa' ya kumaliza tatizo la kukosa penalti na hii ni maandalizi ya kuhakikisha anatumia vyema nafasi hiyo endapo itajitokeza au watafika hatua ya matuta watakapotinga nusu fainali au fainali.

"Nimeanza kutafuta suluhisho, ninaahidi kosa hili halitajirudia tena baada ya kupata dawa yake," alisema Pablo ambaye amechukua mikoba iliyoachwa na Mfaransa Didier Gomes.

Mhispania huyo alisema tayari ameshajua shida ilipokuwa kwa wachezaji wanaopata nafasi ya kupiga penalti na sasa itabaki historia.

"Ni kweli kuna changamoto kwenye upigaji wa penalti, alikosa Bocco (John), Erasto (Nyoni), na Bernard Morrison na Rally Bwalya, tutaendelea kurekebisha, nimeona tatizo kubwa ni kukosa kujiamini tu, nimewajenga kivingine," alisema kocha huyo.

Aliitaja sababu nyingine inayowafanya wachezaji wake wakose penalti ni kushindwa kukaa vizuri wakati wa upigaji jambo ambalo pia ameliboresha.

"Japo kukosa penalti kwa mchezaji sio kitu cha ajabu kwa sababu haina uhakika wa asilimia 100 kufunga, kama kipa ni mzuri na anayejua kumsoma mpigaji. Tunahitaji kushinda na kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, itasaidia kujenga morali kwa wachezaji wangu tutakaporejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Pablo.

Aliongeza malengo ya Simba ni kufanya vizuri katika kila shindano ambalo wanashiriki na kwa mwaka huu wamepanga kuwapa furaha mashabiki wao kuanzia michuano hii.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >